# ETIMOLOJIA YA MAJINA YA MAHALI YA KASKAZINI PEMBA KUWA UTAMBULISHO WA UTAMADUNI WA WAPEMBA

**ZUWENA SULEIMAN ZUBEIR**

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA KWA AJILI YA KUTIMIZA BAADHI YA MASHARTI YA SHAHADA YA UZAMILI YA KISWAHILI (M.A KISWAHILI - ISIMU) YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA**

**2015**

# UTHIBITISHO

Aliyetia saini hapa chini anathibitisha kuwa ameisoma tasnifu hii yenye mada isemayo: ***Etimolojia ya Majina ya Mahali ya Kaskazini Pemba Kuwa Utambulisho wa Utamaduni wa Wapemba*.** Ni tasnifu iliyowasilishwa kutathminiwa kwa azma ya kutimiza masharti ya mahitaji ya shahada ya uzamili ya Kiswahili katika Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.

……………………………………….

Dkt. Anna M. Kishe

(Msimamizi)

……………………..…………….

Tarehe

## HAKI MILIKI

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kutafsiri, kupiga chapa au kutoa tasnifu hii kwa njia yeyote ile bila ya idhini ya mwandishi au idhini ya Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania kwa niaba ya mwandishi.

# TAMKO

Mimi **Zuwena Suleiman Zubeir,** natamka ya kwamba hii ni tasnifu yangu mwenyewe na kwamba haijawahi kuwasilishwa na wala haitawasilishwa katika chuo kikuu kingine chochote kwa ajili ya mahitaji ya kutunukiwa shahada kama hii au shahada nyengine.

…………………………………………………

Saini

……………………………………………….

Tarehe

# TABARUKU

Naitunuku kazi hii kwa Baba yangu mzazi Bwana Suleiman, mama yangu Bi. Mgeni Moh'd. Pia na watoto wangu Aysar, Suleiman na Ali ili kwao iwe ni chachu ya kuthamini kujali na kutafuta elimu kwa bidii.

## SHUKURANI

Kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu Muumba wa viumbe wote na mtukufu wa daraja kwa kunijaalia uwezo wa kufanya utafiti, kuandika na kunithibitisha katika kuikamilisha kazi hii nikiwa na afya njema. Pili napenda kutoa shukurani zangu kwa wahadhiri, washauri waelekezaji na wawezeshaji wafuatao: Kwanza kabisa kwa msimamizi wangu Dkt. Anna. M. Kishe kwa namna mbali mbali aliniongoza na kusimamia kwa moyo wake wote wa kujitolea hadi kukamilisha kazi hii.

Pili kwa wahadhiri wangu wote wa kitivo cha sanaa na sayansi za jamii kwa kunielekeza na kunishauri katika muda wote wa masomo. Vile vile shukurani zimwendee maalim Bakar Kombo kwa kuniongoza na kunielekeza kwa jitihada zote na wakati mwingine kukemea lakini mchango wake ndio uliopelekea kumalizika kwa kazi hii.

Shukurani za dhati ziwaendee wazazi wagu wapendwa walitoa mchango mkubwa wa hali na mali mpaka kuikamilisha kazi hii. Kadhalika shukurani za pekee zimwendee mume wangu Bwana Nassor. A. Salim kwa kuniruhusu kusoma na kustahamili shida zilotokana na harakati zote za masomo, utafiti na uandishi wa kazihii hadi kumaliza. Mwisho napenda kuwashukuru wanafunzi wenzangu wote wa shahada ya uzamili kwa mashirikiano yao kwa muda wote wa masomo, pamoja na wote walionisaidia kazi hii kwa namna moja au nyengine hadi kukamilika kwake. Wote kwa pamoja nawatakia kila lenye kheri.

# IKISIRI

Utafiti huu ulihusu Etimolojia ya majina ya mahali. Ulichunguza etimolojia ya majina ya mahali ya Kaskazini Pemba kuwa utambulisho wa utamaduni wa Wapemba. Mtafiti aliongozwa na malengo matatu. Kwanza, kubainisha etimolojia ya majina ya mahali yanayopatikana Kaskazini Pemba; pili, kufafanua vigezo vinavyotumika kutoa majina ya mahali ya Kaskazini Pemba; na tatu, kubainisha utamaduni wa Wapemba jinsi ulivyoakisiwa na majina ya mahali ya Kaskazini Pemba. Ili kufikia lengo kuu lililokusudiwa mbinu mbali mbali za utafiti zilihusika. Mbinu hizo ni pamoja na mahojiano, hojaji pamoja na mjadala wa vikundi. Utafiti huu uliongozwa na nadharia jumuishi ambayo iliakisi data za utafiti huu kutokana na maoni yaliyotolewa na watafitiwa na wanajamii kwa ujumla yaliunda data za utafiti huu. Kwa upande wa matokeo ya utafiti, mtafiti aligundua kuwa majina ya mahali yana mfungamano na jamii na utamaduni wa jamii husika. Baadhi ya majina yanaakisi moja kwa moja shughuli wanazofanya wanajamii. Pia amebaini kuwa baadhi ya majina huwa ni ya hali ya kimazingira ya maeneo hayo kama jiografia inavyoonekana. Hata hivyo kuna majina ya mahali hutokana na watu maarufu au matendo ya kihistoria yaliyofanywa na wakazi wa zamani wa maeneo hayo. Mtafiti katika kazi yake amegundua pengo ambalo linahitaji kufanyiwa kazi, uibukaji wa majina mapya yanaathiri utamaduni wa jamii. Mtafiti anapendekeza kufanyika kwa utafiti utakaoeleza sababu zinazopelekea kuibuka kwa majina mapya ya mahali. Na pia maumbo ya majina ya mahali katika kipengele cha mofolojia na fonolojia kinaweza kufanyiwa utafiti kuona jinsi majina ya mahali yalivyo na maumbo mbali mbali.

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.1 Utangulizi wa Jumla

Utafiti huu unahusu etimolojia ya majina ya mahali Kaskazini Pemba kuwa utambulisho wa utamaduni wa Wapemba. Utafiti huu ulifanyika katika eneo la Kaskazini Pemba. Pemba ni kisiwa kilicho pembezoni mwa mwambao wa pwani ya Afrika Mashariki; kwenye bahari ya hindi. Kisiwa hiki kina takribani kilomita hamsini (50). Kiko Kaskazini Mashariki ya kisiwa cha Unguja na kilomita hamsini Mashariki ya pwani ya Tanganyika. Kisiwa hiki kina historia ndefu inayohusiana na kuishi ya ukaaji binadamu. Wakazi wa kisiwa hiki, kazi zao za asili, ni ukulima mdogo mdogo. Mazao mashuhuri ya chakula yanayozalishwa kisiwani humo ni mpunga, muhogo, maharage chooko na kunde. Pia watu hawa hujishughulisha na sehemu za uvuvi. Mji mkuu wa kisiwa cha Pemba ni Chake chake uliojitenga juu ya kilima. Magharibi ya mji wa Chake chake kuna kisiwa mashuhuri kwa maswali ya utalii kiitwacho Misali.

Kimgawanyo Pemba ina mikoa miwili mikubwa nayo ni mkoa wa Kaskazini na mkoa wa Kusini. Mkoa wa Kaskazini una wilaya mbili wilaya ya Wete na wilaya ya Micheweni , na mkoa wa Kusini una wilaya mbili wilaya ya Mkoani na wilaya ya Chake. Pemba ina majimbo kumi na nane (18) ya uchaguzi kama yalivyotumika katika uchaguzi wa mwaka (2010).

Kwa asili Wapemba ni watu wenye asili ya uzawa wa kisiwa cha Pemba. Lugha wanayozungumza ni Kiswahili. Kiswahili kinachozungumzwa na Wapemba kinaitwa ‘Kipemba’. Ni moja ya lahaja za Kiswahili kinachozungumzwa kisiwani Pemba

pekee. Khamis katika BAKIZA (2008) akiwanukuu Chiraghdin & Mnyampala (1977) na Nurse & Spear (1985) kuhusu lugha ya Waswahili anasema: *"...lugha ya Waswahili ni Kiswahili chenye kujumuisha Viswahili au Lahaja zake 16 zikiwemo 1. Kiunguja Mjini (Unguja mjini Magharibi na Kati). 2. Kipate (Kaskazini ya Pate). 3. Kisiu (Mji wa Siu Kenya). 4. Kibajuni au Kitikuu (Kaskazini ya Lam na Kusini ya Kismayuu-Shungwaya). 5. Kimgao au Kimwani (Kilwa na Kaskazini ya Mozambique). 6. Kimtang'ata (Tanga mjini na Pangani). 7. Kipemba (Kisiwa cha Pemba). 8. Kimvita (Katikati ya Mombasa). 9. Kijomvu (Kaskazini ya Mombasa). 10. Kiamu (Kisiwa cha Lamu). 11. Kimrima (Mafia, Rufiji na Dar es Salaam). 12. Kimakunduchi (Kusini Unguja). 13. Chimiini au Chimbalazi au Kibarawa (Barawa). 14. Kitumbatu (Tumbatu na Kaskazini Unguja). 15. Kichichifundi au Chifunzi (Kusini ya Gaza hadi Wasin, Kenya)* na *16. Kingazija (Komoro)".*

Utamaduni wa Wapemba ni utamaduni wa mswahili wenye kujengwa na mila na desturi halisi za Waswahili. Khamis katika BAKIZA (2008) anabainisha kuwa *"Mila za Waswahili ni juu ya yale waliyoyaamini kuwa yanawaletea upendo wa kuishi kijamaa, kimitaa au kivijiji. Mfano, kula kiukumbi, kuabudu pamoja na kusaidiana kiuvyawa au kiujima kwa malezi, uuguzi, ndoa, tiba wakati wa misiba...Waswahili wana mila ya kuoa mke mmoja hadi wanne…Pamoja na imani ya dini ya Kiislamu baadhi ya Waswahili wana mila za kufanyiana uchawi kwa lengo la kuhusudiana kwa kurogana, kupeana punju, mashetani, majini, kupelekeana chui, vizuu na kuwangiana…"*

*"Kimavazi, Waswahili wana dasturi ya mavazi changamano, ambayo ni pamoja na shati, shuka, suruali, kanzu, kofia za viua, au mfuto, viatu vya miti, mipira au ngozi*

*kwa wanaume. Wanawake mavazi yao ni kanzu, shumizi, buibui, kanga, kaniki, mera, gwaguro, mitandio, sidiria na viatu vya ngozi. Wanawake wa Kiswahili zaidi ya mavazi hayo wana desturi ya kujipamba kwa vyombo vya dhahabu, fedha au kareti kama bangili, vidani, vipini, pete na herini. Aidha hutengeneza vikuba na mapambo mengine kwa kutumia maua yanayonukia kama mkadi, asumini, viluwa au mawaridi. Wanawake hawa hujitona kwa hina na podari, kujipura kwa behedani, rangi za midomo, mafuta mazuri ya haliudi, tarabizuna, miski pamoja na kujifukiza udi wa mawaridi pale wanapokua nyumbani, wanapokwenda harusini, safari ya matembezi au hata kazini.*

Shughuli kuu za watu hawa ni uvuvi, ufugaji, kilimo na biashara. *Kwa upande wa vyakula Waswahili wana dasturi ya kula vyakula vya nazi kama vile wali, muhogo, viazi vikuu, viazi vidogo, mashelisheli, ndizi na majimbi. Dasturi ya Mswahili kwa upande wa vyakula haikuishia hapo, wakati mwingine hutumia ustadi wake kwa kupika vya mchanganyiko/msambwija kama wa viazi vikuu kwa muhogo, maboga kwa viazi vitamu, kunde kwa muhogo na vyenginevyo.*

## 1.2 Usuli wa Mada

Majina ni mojawapo ya kategoria ya maneno ambayo imeshughulikiwa na wataalamu wengi. Kati ya hao ni, Mgullu (1999), Massamba (2004), Khamisi (2010), Saluhaya (2010). Kihore na wenzake (2008) wameeleza jina ni aina ya neno linalotaja au kubainisha viumbe hai, vitu visivyo uhai, mahali, hisia, hali, maarifa au tukio katika tungo. Ally na wenzake (1930) wamefafanua kwamba jina ni kila analoitwa mwanadamu, mnyama, mmea, vitu vigumu au kitu kingine chochote. Kwa mujibu wa kazi hii mtafiti amelifasili jina kuwa ni neno linalotaja vitu, viumbe, hisia

au hali ili kuvitofautisha na vingine. Kihore (2009) ametaja aina tatu za majina ambazo ni majina jumuishi, majina ya pekee na majina ya kikundi. Pamoja na yote hayo wameeleza kuwepo kwa majina ya kawaida kama vile kiti, daftari, kalamu. Majina ya pekee ambayo huwa na umbo na tabia ya kipekee au mahususi, majina haya yanaweza kuwa ya watu, mfano, *Ahmad, John, Khamisi*; majina ya mahali, mfano, *Wingwi, Tumbe, Limbani, Ole. Kinyasini, n.k.* Ni kweli kwamba *Ahmad* wako wengi Duniani lakini kila mmoja yuko tofauti na mwingine kutokana umbo ama tabia. Halikadhalika Kinyasini zipo Unguja na Pemba lakini ni kinyasini mbili zinaztofautiana kimazingira na asili yake.

Majina ya *mahali* ni aina moja wapo ya majina ya pekee. Majina haya yanataja miji na mitaa (kwa maeneo ya mjini) au vijiji (kwa maeneo ya shamba). Mfano, katika mji wa *Wete* kuna majina ya mitaa kama *Limbani*, *Kizimbani na Bopwe.* Kila jina lina asili yake. Wataalamu mbali mbali walitafiti majina ya mahali, miongoni mwao ni Boas (1964) Schotsman (2003) wanaeleza vigezo vya utowaji wa majina ya mahali katika jamii. Mutembei (2009:31) anauliza kwa nini watu hutoa majina ya vitu, mahali, watu au matukio? Je, ni utambulisho au kiaelelezo cha yaliyopita au ni utabiri wa yatakayotokea? Akijibu maswali hayo Mutembei (keshatajwa) anaeleza kuwa, kwa vyovyote vile kuna msukumo unaowafanya watu watoe majina. Majina tunayopewa huwa ni utambulisho wa asili zetu, kwa kumtambulisha mtu, eneo analotoka, tabia na sifa zake na humtofautisha mtu mmoja na mwingine. Kwa kuwa lugha inamhusu mwanadamu, maisha yake, kazi zake, migogoro yake na jinsi anavyoishi ndani ya mazingira yake. Buberwa (2010) anaeleza vigezo vya utoaji majina ya mahali katika jamii alitafiti maana zinazoambatana na majina ya mahali.

Hivyo majina ya *mahali* ni mojawapo ya maneno yanayotumiwa na wanajamii katika shughuli zao za kila siku, ni kipengele chenye umuhimu mkubwa kwa wanajamii kwani hutambulisha utamaduni wao, kujua asili yao na kujua maana zilizomo ndani ya majina. Kwa maana hiyo, mtafiti amechagua mada hii ili aweze kuchunguza etimolojia ya majina ya mahali na jinsi yanavyotumiwa kutambulisha utamaduni wa jamii. Kwa kuchunguza asili ya majina ya mahali yanayopatikana Kaskazini Pemba na kueleza sababu za majina ya mahali.

## 1.3 Tamko la Tatizo la Utafiti

Suala la majina ya mahali limetafitiwa na wataalamu wengi wakiwemo wageni na wenyeji wa Tanzania. Tafiti nyingi zimebainisha kuwa kuna mambo mengi yanayochangia kuwepo kwa asili ya majina ya mahali, zikiwemo sababu za kijamii, kisiasa na kiutamaduni. Mlacha (1995) alieleza majina ya mitaa ya Kaskazini Pemba na chanzo chake, mfano, Uvuani limetokana na utamaduni wa kuvua; Salim (hajapishwa) alibainisha majina ya mahali kama vile Ndagoni. Pia, majina ya mahali yametokana na maingiliano ya wageni na wenyeji wa Asia na India. Aliongeza kuwa katika kueleza historia na utamduni wa Waswahili wa mwambao majina kama Malindi, Kiwayu, Pemba na Uziwa yana asili ya Uswahili. Mlacha (keshatajwa) anaeleza kuwa majina ya mahali ya Waswahili yanaakisi kumbukumbu za yaliyopita yanayohusiana na mambo ya kisiasa au maswali ya kijamii. Katika kuchunguza maumbo ya majina ya mahali katika Kiswahili aligundua kuna viambishi awali katika baadhi ya majina.

Pamoja na wataalamu hao kuchunguza majina ya mahali na asili zake katika jamii mbalimbali, lakini kwa kiwango anachoelewa mtafiti bado tafiti zinazoelezea kwa

undani asili ya majina ya mahali katika mkoa wa Kaskazini Pemba na kuyahusisha na masuala ya utambulisho wa asili ya wanajamii au utamaduni wao hazijafanywa. Kwa mfano, Mlacha (keshatajwa) ametumia fasihi simulizi kuchunguza asili ya majina ya maeneo na kwamba kazi yake imeegemezwa kwenye fasihi kuliko isimu. Wataalamu wengine wameelezea kuhusu utamaduni wa Wapemba pasipo kuuhusisha na vigezo vya kiisimu. Kwa muktadha huo, mtafiti ameshawishika kufanyia utafiti eneo hili, ili kugundua asili za majina na kwa vipi majina hayo yanaakisi utamaduni wa jamii?

## 1.4 Malengo ya Utafiti

Haya yamegawika katika lengo la jumla na malengo mahususi.

### 1.4.1 Lengo la Jumla la Utafiti

Kuchunguza etimolojia ya majina ya mahali ya Kaskazini Pemba kuwa utambulisho wa utamaduni wa Wapemba.

### 1.4.2 Malengo Mahususi

i) Kubainisha etimolojia ya majina ya mahali yanayopatikana Kaskazini Pemba.

ii) Kufafanua vigezo vinavyotumika kutoa majina ya mahali ya Kaskazini Pemba.

iii) Kubainisha utamaduni wa Wapemba jinsi ulivyoakisiwa na majina ya mahali ya Kaskazini Pemba.

### 1.4.3 Maswali ya Utafiti

i) Ni ipi etimolojia ya majina ya mahali yanayopatikana Kaskazini Pemba?

ii) Ni vigezo vipi vinavyotumika kutowa majina ya mahali ya Kaskazini Pemba?

iii) Ni upi utamaduni wa Wapemba unaojitokeza kutokana na majina ya mahali ya Kaskazini Pemba?

## 1.5 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu utasaidia katika nyanja tofauti za kitaalamu. Kwanza, utasaidia kinadharia kwa kukuza lugha kutokana na kuongeza maana tofauti zinazofungamana na majina ya mahali ambapo watumiaji walikuwa hawajui. Pili, utafiti huu utatoa mchango mkubwa katika nyanja ya utamaduni kwa kuwafumbua macho wanajamii walio wengi kwa kuwatambulisha mambo yaliyohusu tamaduni zao za asili. Tatu, utafiti huu utakuwa ni chanzo kimojawapo cha viongozi wa serikali kuweka kumbukumbu na kuweka mkazo wa kuenzi majina ya asili. Nne, utafiti huu utatoa mchango kwenye nyanja ya taaluma ya isimu kama marejeleo ya fani hiyo kwa kuonesha jinsi lugha inavyotumika kuitambulisha jamii.

### 1.5.1 Changamoto za Utafiti na Utatuzi Wake

Kulikuwa na changamoto kadhaa ambazo zilijitokeza katika utafiti huu, baadhi ya changamoto hizo ni:

Tatizo la upatikanaji wa watafitiwa: Wakati wa kukusanya data watafitiwa wengi walikuwa katika shughuli zao za kujikimu kimaisha, hivyo mtafiti alilazimika kutafuta muda mwingine ambao aliweza kuwapata bila kuwasumbua.

Tatizo muda: Kazi ya utafiti ni ngumu na ni yenye kuendelea na wala haina kiwango maalumu cha muda. Kutokana na mahitaji ya kitaaluma hapana budi ikamilike kwa muda uliopangwa. Jambo hili lilikuwa changamoto kwani ufinyu wa muda uliathiri

ukusanyaji wa data na kuwapata watafitiwa. Hivyo mipango ilifanyika ya kuwatumia masheha kuwatafuta walengwa na kutupangia muda ambao uliwezesha kufanikisha zoezi la utafiti.

Tatizo la mbinu: Mbinu ya mahojiano ilitumika lakini ilikuwa changamoto kwani wahojiwa walikuwa wanaingiza hisia zao za kisiasa walipohojiwa asili ya majina, mtafiti aliyadhibiti kwa kuwarudisha katika mada iliyokusudiwa, na piawalikua wagumu kutoa mila zao kwa kuchelea kurikodiwa. Mtafiti aliwapa maelekezo na kuwaondoa wasi wasi na kuwahakikishia usalama wao ikiwa ni moja ya maadili ya utafiti.

Pia mtafiti alipata vikwazo katika kukusanya data ambapo baadhi ya wahojiwa walikuwa wanakosa mwelekeo, hawana kumbukumbu sahihi, kutokana na kutojua umuhimu wa historia, mtafiti alitumia watoto wao kuwakumbusha kwa kuwauliza maswali ya nyongeza ili kuvuta kumbukumbu ya wazee hao.

## 1.6 Hitimisho

Sura hii imeeleza vipengele mbali mbali kama vile usuli wa tatizo,malengo ya utafiti,maswali ya utafiti,umuhimu wa utafiti,changamoto za utafiti na tatizo la uatafiti.

# SURA YA PILI

# UTALII WA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA

## 2.1 Utangulizi

Sura hii inazungumzia maandishi mbali mbali yaliyoandikwa kuhusu mada hii. Mtafiti alipitia maandishi ya wataalamu na watafiti mbali mbali yenye ukaribu na mada hii. Pia ameeleza nadharia iliyoongoza utafiti huu.

## 2.2 Mapitio kuhusu Majina na Aina Zake

Dhana ya majina ni pana na imeandikiwa na wa taalamu wengi wa fani ya Isimu. Utafiti huu unajihusisha na uchunguzi wa etimolojia za majina, hivyo majina ndio ajenda inayoangaliwa kwenye utafiti huu.Miongoni mwa wataalamu walioangazia eneo hili ni pamoja na hawa wafuatao:-

Kama wasemavyo Kihore na wenzake (2008), kwamba jina ni aina ya neno linalotaja au kubainisha viumbe hai, vitu visivyo uhai, mahali, hisia, hali, maarifa au tukio katika tungo. Katika sehemu hiyo, Kihore (keshatajwa) ameanisha aina tatu za majina ambazo ni: i) Majina jumuishi ambayo pia huitwa majina ya kawaida ii) Majina Mahususi na majina ya jamii ambayo pia huitwa majina ya kikundi. Kapinga (1983) kwa upande wake ameainisha aina saba za majina, kama iliyoorodheshwa na mtafiti hapo chini. i) Majina ya pekee ii) Majina ya kawaida iii) Majina ya Dhahania iv) Majina ya mguso v) Majina ya kitu kimoja kimoja vi) Majina ya jamii vii) Majina ya wingi. ameainisha aina (6) za nomino i) Nomino za pekee ii) Nomino za kawaida iii) Nomino za Mguso iv) Nomino za dhahamia v) Nomino zinazohesabika

na zisizohesabika vi) Nomino za jamii. Mgulu (1999) ameainisha aina sita za nomino i) nomino za pekee ii) nomino za kawaida iii) nomino za mguso iv) nomino dhahania v) nomino zinazohesabika na zisizohesabika na vi) nomino za jamii. Nyangwine na Massebo (2006) wameziainisha aina tano za nomino. i) Nomino za pekee ii) Nomino za kawaida iii) Nomino za Dhahania iv) Nomino za jamii v) Nomino za wingi. Tukichunguza tutagundua kuwa wataalamu wote hawa, pamoja na kutofautiana kuhusu aina za majina wamekubaliana kuwepo kwa majina ya pekee ambayo sana huhusisha mahali na maumbile ya kijiografia.

Kapinga (keshatajwa), ameeleza kuwa majina ya pekee ni kama vile Majina ya watu mfano Khamis, Maria, Songambele, Taabu. Majina ya mahali kwa mfano, ni kama vile Tanga, Dodoma, Kilimanjaro. Majina ya siku za Juma kama Jumatatu, Jumanne, Jumatano na kadhalika pia yanaingia katika eneo hili. Majina ya miezi Januari, Febuari, Marchi, na kadhalika ni kipengele kinachohusu pia eneo hili.

Mgullu (keshatajwa) anasema“Nomino za pekee ni nomino ambazo hutaja vitu vya pekee. Kitu cha pekee ni kitu mahususi na ni cha pekee kwa sababu kipo chenyewe tu. Anaendelea kusema hapa duniani, Nomino za pekee hutaja majina ya Watu: Tuma, Omar, Tumaini; Miji: Nairobi, Dodoma, n.k Nchi: Kenya, Tanzania, Zambia, n.k Mito: Tana, Rufiji, n.k Maziwa: Victoria, Tanganyika n.k Milima: Elgon, Kilimanjaro, n.k Bahari: Hindi, Atlantiki, n.k.

Majina ya mahali kwa uainishaji uliotajwa hapo juu ni sehemu ya majina ya pekee. Hii ndiyo aina ya majina anayoshughulikia mtafiti wa kazi hii. Ukichunguza kwa

makini utagundua kwamba majina hayo yamebeba maana inayotokana na utamaduni na mazingira ya jamii husika. Majina ya wa mahali hubeba maana mbali mbali ambazo kimsingi hueleweka kwa wanajamii watumiaji wa lugha wenyewe kutokana na kuwa na maarifa elimu na uzoefu wa maisha unaofanana**.**

Pia majina haya huwa na sababu maalumu za kutolewa, inawezekana kutokana na matukio, historia, utamaduni ama athari mbali mbali zinazotokana na familia au jamii kwa ujumla. Maelezo ya wataalamu yanayohusu majina na aina zake yana mchango mkubwa kwa mtafiti, kwani alipokuwa akikutana na jina la mahali aliweza kubainisha kiasili jina hilo liliktokana na kundi lipi miongoni mwa makundi ya aina za majina.

## 2.3 Kazi Tangulizi Zinazohusu Majina ya Watu na Asili Zake

Katika kazi zilizopitiwa hapa ni zile zinazohusu majina ya watu na maana zake pamoja na kazi zilizoeleza vigezo vilivyotumika kutolea majina ya watu. Omary (1970) anaeleza majina ya watu katika jamii ya *Chasu* na anasema kwamba, majina ya watu yanatokana na vigezo kama mwingiliano wa jamii za kigeni, hali ya kipato, sura ya nchi pamoja na matukio fulani kama vile vita.

Ametoa mifano ya majina kama ya “Sekona” na “Nankonda” akasema kwamba “Sekona” ni mtoto wa kiume aliezaliwa wakati wa vita, na “Nankonda” ni mtoto wa kike aliezaliwa wakati wa vita. Omary (keshatajwa) ameendelea kusema kwamba, Katika kipindi cha jando na unyago, “Mshitu” wa msitu, ni jina analopewa mwanamme, wakati ambapo “Namshitu” wa msitu, ni jina analopewa mwanamke. Utafiti wa Omary (keshatajwa) haukuchunguza majina ya mahali, lakini

umemuongoza mtafiti kugundua kuwa majina huwa yana asili ya kuitwa kwake. majina huwa yana asili ya kuitwa kwake. Baver (1979) katika uchunguzi wake wa namna ya utoaji wa majina kwa jamii ya Wachina, alibaini kuwa mtu mmoja hupewa majina katika nyakati tofauti. Kwanza, hutolewa kipindi cha utoto, hutolewa akiwa shuleni, baada ya kuoa, hutolewa kwa kuzingatia nafasi yake ya kazi na jina la utani.

Kwa hivyo falsafa ya utoaji majina huashiria kutambuliwa kwa kazi za namna mbalimbali, hadhi yake au madaraka ambayo mwenye jina huwa nayo pamoja na ushirikiano wake na watu waliokuwepo zamani na waliopo sasa. Majina haya huashiria mabadiliko ya tabia kutokana na uzoefu wake wa maisha, nafasi yake, mafanikio na mashaka anayokumbana nayo maishani.Kazi hii haikuchunguza majina ya mahali lakini ilimsaidia kuona jinsi majina yanavyoweza kufanyiwa uchunguzi wa kisayansi na nadharia kwani majina ya pekee yana sifa fulani zilizo na upekee na ndio mtafiti akatumia kazi hii kuhusisha na mada yake ya majina ya mahali ikiwa ni moja ya majina ya pekee.

Naye Chulk (1992) alitafiti majina ya watu wa Afrika ambapo alieleza kuwa kawaida watu hupewa majina kutokana na matukio fulani, vitu vikubwa vya kushangaza, siku au juma mtu alipozaliwa. Mfano "Aiende", Kiyoruba lina maana ya tuliyekuwa tumemuomba/tunamsubiri. Jina hili limetokana na familia ambayo muda mrefu haijapata mtoto wa kiume. Utafiti huu umechunguza majina ya watu na sio ya mahali, hata hivyo umemsaidia mtafiti kugundua kuwa katika majina kuna maana zinazojificha na hujulikana na jamii au familia yenyewe tu.Ingawa kazi ya Chulk (keshatajwa) haikujadili majina ya mahali lakini imetoa mchango wa utafiti huu

kugundua maana za majina ambazo wanazijua wanajamii wenyewe tu. Kazii hii imemuongoza mtafiti kuhusisha mada yake na iliyotangulia.

Rubanza (2000) alitafiti majina ya watu katika Kihaya na Kiyoruba. Zaidi yeye alichunguza ubunifu wa kiisimu uliomo na alieleza kuwa majina yanazingatia mazingira ya kuzaliwa kwa mtoto, mfuatano wao katika kuzaliwa na migongano katika jamii na muundo wa familia. Matokeo ya utafiti wake yanaonesha kuwa majina ya watu yanabeba ujumbe unaokubalika na jamii. Maelezo haya yanaonesha kuwa majina huwa yanabeba maudhui fulani katika jamii naye pia hakuchunguza majina ya mahali.. Utafiti huu ulimsaidia mtafiti kugundua kuwa majina hutokana na utamaduni wa jamii husika.

Kofi (2006) anaeleza kuwa majina ya Waakani hubeba ujumbe unaotambulisha muktadha wa kijamii. Dai hili limesimamia hoja ya kwamba majina si ya kinasibu bali yanatokana na utamaduni wa muktadha wa wazungumzaji wa jamiilugha hiyo. Majina ya watu yanawakilisha namna watu wanavyoishi na kuheshimu mifumo ya tamaduni zao. Hivyo utafiti wake ulilenga kuchanganua maana za majina kisemantiki, na matokeo ya utafiti wake yalionesha majina hutolewa kwa kuzingatia vigezo mbali mbali. Vigezo hivyo ni pamoja na siku aliyozaliwa mtoto, majina ya familia, majina yanayofanana na majina ya mimea, wanyama na majina yanayojumuisha majina ya utani, makundi ya wahalifu, majina yanayotokana na imani za nguvu za asili, na shughuli mahususi. Mfano, mtoto wa kiume aliyezaliwa siku ya Jumatatu, alipewa jina la "Kwadwa" na mtoto wa kike aliitwa *"Adwoa".* Kofi (keshatajwa), anaendelea kusema kuwa Waakani wanaamini kuwa jina linafungamana na nguvu za asili na hutarajiwa kuwa ama kielelezo na kiwakilishi

hasi au chanya cha maisha na tabia za watu. Jina la mtu ni wajibu wa jamii nzima, yaani huhusiana na utendaji na ushiriki wake katika jamii.

Msanjila na wenzake (2009) wanaeleza kuwa majina mengi ya familia hutolewa kwa lugha inayozungumzwa na jamii husika hivyo, hubeba maana inayotambuliwa na jamii husika.Wametoa mfano wa majina ya watu na matukio, kama vile jina la Chonya Magulu linatokana na tukio la njaa lililotokea mwaka (1980), ambalo lilidhoofisha miguu na watu na watu wengi kushindwa kutembea. Matonya amezaliwa wakati wa mvua.

Msanjila na wenzake (2009) wamezungumzia juu ya majina ya watu katika jamii ya Wagogo. Matokeo ya utafiti wa Msanjila na wenzake (keshatajwa) Unaonesha kuwa majina yanatambulisha jamii na kubaini kwamba majina hayo ya jamii ya Wagogo yanawakilisha matukio yanayotokea katika jamii hiyo.Waliendelea kusema kuwa majina ya watu huwa na maana mbali mbali ambazo kimsingi zinaeleweka na jamii husika. Katika kutoa mifano ya majina walichukua majina ya Wagogo waishio Dodoma nchini Tanzania kwa mfano: Jina la “Manzala” lina maana ya mtoto wa kike aliyezaliwa wakati wa njaa. Iicha ya kuwa jina lina maana, mtu anaweza kupewa jina la aina hiyo kwa sababu ya kurithi tu kutoka kwa babu au kwa bibi yake na sio kwa sababu amezaliwa katika kipindi kinachohuisiana na jina alilopewa. Kwa maana hiyo mtu anayetumia majina ya namnahii akiwa popote atatambuliwa kwamba anatoka katika jamii ya Wagogo.

Manyasa(2010) anaeleza vigezo vitumikavyo kutolea majina ya watu katika jamii ya Wasukuma. Ameeleza kwamba, baadhi ya majina hutokana na matukio yaibukayo

kwenye kipindi cha kuzaliwa mtoto. Mfano, “vita” huzuwa majina kama “Nshilikale” ni mtoto aliyezaliwa kipindi cha vita. Yanaweza pia kutokana na magonjwa makali yanayompata mtoto kipindi cha kuzaliwa kwake. Mfano, "mboku" ni jina la mtoto mwenye uoni hafifu. Pia jina linaweza kutokana na hadhi ya mtu, mfano, "Mtemi" anaweaza kupewa mtoto wa kiume aliyezaliwa kipindi cha utawala wa Mtemi maarufu. Manyasa (keshatajwa) anafafanua kwamba utoaji wa majina unatofautiana kati ya jamii moja na jamii nyingine. Kazi ya Manyasa (keshatajwa) inampatia mtafiti mwongozo wa kugundua kuwa majina hutolewa kwa sababu maalumu za kiitikadi na matendo katika jamii.

Baitan (2010) alizungumzia majina ya watu katika Kihaya. Alisema kuwa majina ya Kihaya yanatokana na matukio fulani, itikadi, jinsi na kadhalika. Mfano, kuna majina wapewayo watoto waliozaliwa mapacha. Kwa mfano jina la “Ishengoma” hupewa pacha wa kiume, aliyetangulia kuzaliwa na jina la“Nyangoma” huitwa pacha wa kike aliyezaliwa mwanzo. Wanaofuata kuzaliwa wakiwa mapacha huitwa “Kato” akiwa mwanamme, au “Nyakato” akiwa mwanamke. Utafiti wa Baitan (keshatajwa) umemsaidia mtafiti wa kazi hii, kugundua maana za majina zinazojulikana na wanajamii wenyewe. Pia kumuongoza katika kupata data inayohusu majina na utambulisho Kwa Kutilia mkazo wanajamii na utambulisho.Maelezo hayo yalimsaidia mtafiti kugundua maana za majina na ufungamano wa jamii.

## 2.4 Kazi Tangulizi Zinazohusu Majina ya Mahali

Cameroon (1961) anaeleza utoaji wa majina ya mahali katika jamii ya Waingereza. Ametoa aina mbili; yale ya makazi na yale ya sura ya nchi ya eneo hilo. Mfano, ‘Greenhill’ ikimaanisha eneo lenye kilima chenye rangi nyingi ya kijani. Kazi ya

Cameroon (keshatajwa) ilimpa mtafiti kujua maeneo yapi yamefanyiwa utafiti kuhusu mada yake, ilimsaidia kugundua majina ya mahali yaliyotafitiwa zamani na katika jaimii tofauti kazii hii imetofautika na ya cameroon kwa vile imejikita zaidi kwenye utamaduni wa jamii ya kaskazini Pemba.

Hymen (1964) anaeleza kuwa majina ya mahali yanaakisi fikra, watu pamoja na vipengele vya utamaduni. . Chum (1982) anaeleza asili ya mitaa inayopatikana Mkoa wa Kusini Unguja. Anataja majina kama vile *Paje* ambayo asili yake ni mnyama aitwe paa, pamoja na kilimo cha chooko. Anasimulia kwamba, miongoni mwa wageni waliofika Unguja walikuwa ni ndugu saba ambao walishauriana kuishi pembezoni mwa pwani ya Unguja ili waendeleze kilimo cha chooko. Wakati wakijadiliana mmoja aliuliza tukiwa na kilimo hiki paa je? kwa vile paa wanapenda chooko. Kazi hii ilimpa dira mtafiti la kugundua tafiti zilizofanywa ni asili ya vijiji nasi majina ya mahali yanavyoakisi utamaduni wa jamii kama kazi ya utafiti huu ilivyojipambanua.

Mlacha (1995) anaeleza asili ya majina ya mitaa inayopatikana kisiwani Pemba. "Uvuani" asili yake walihamia wageni wakawa wanafanya shughuli za uvuvi, wakaja watu wakawauliza Uvuani, yaani unavua nini? Hapo ndipo kijiji hicho kikaitwa Uvuani. *"Micheweni*" walikuwepo watu makatili wenye tabia ya kuwaua watu kutokana na imani za kichawi. Hivyo watu walioishi mbali na eneo hilo walipaita michawini linatokana na Uchawini lenye maana ya kuuwa, baadaye pakaitwa Micheweni. Kazi hii imesaidia mtafiti kupata ushahidi wa asili ya majina hayo.

Rey (1995) anaeleza kwamba majina yanayotumika kutambulisha watu au mahali yanaonesha utofauti baina ya jamii moja na nyingine, kutokana na vigezo vya asili, historia na utamaduni. . Pia kwa upande wake Muzale (1998) anasema kuwa ingawa utoaji majina ni tukio la asili kwa jamii zote lakini kuna tofauti katika ubainishaji wa hayo, maana za majina hayo nazo hutofautiana toka jamii moja na nyingine. Hivyo, matukio yanayohusika kutoa majina ya mahali toka jamii moja na nyingine hayawezi kufanana kwani kila jamii ina taratibu zake. Utafiti wa Muzale (keshatajwa) unamuongoza mtafiti kugundua kuwa upo utofauti wa kazi yake na zilizotangulia kwani wamechunguza vigezo vya utoaji majina na maana za majina lakini kazi hii inahusisha majina yanavyoakisi utamaduni wa wanajamii wa mahali hapo.

Abuubakar (1998) ameeleza mtaa wa mtoni umepewa jina hilo kutokana na jengo kongwe la Sultani wa Zanzibar lililokuwepo pembezoni mwa mto mdogo uliotokea upande wa ndani wa kisiwa cha Unguja,uliopitisha maji yake masafa mafupi baada ya kulipita jumba hilo kuelekea pwani.Pialieleza jina la Chuini, kulikuwa na jumba kubwa lenye bustani kubwa ambapo walikuwa wakifugwa wanyama kama chui, simba na wengineo.

Scotsman (2003) anaeleza historia ya maana ya majina ya mahali katika jiji la Dar es Salaam. Alitumia majina ya vituo vya daladala na majina ya mitaa/kata. Alieleza majina ya vituo vya mabasi yanatokana na majengo kama shule, hospitali, makanisa, watu maarufu, shughuli zinzofanywa na watu katika eneo hilo na uelekeo kituo kilipo, mfano, njia panda kwa Kawawa. Kituo hiki kipo njia inayoelekea kwa Kawawa. Pia anaeleza majina ya mitaa yanatokana na mimea iliyopo katika sehemu hiyo, lugha za asili, mfano, “Mwananyamala” yaani ‘mtoto usilie’, ni neno la

Kizaramo lililotolewa na wanawake walioishi awali katika eneo hilo kutumia usemi huu wakati wakibembeleza watoto wakiwa katika shughuli za shambani. Mengine hutokana na maeneo ambayo yanashabihiana, mfano, Mawezi ya Dar es Salaam ni eneo la mteremko kama ule wa "Mawenzi" ya Kilimnjaro.

Masoud (2005) ameeleza asili ya jina la Mtende: Kuwa watu wa Makunduchi walienda kutembea kijiji cha jirani wakawakuta wenyeji wa huko wamelima mazao mengi, wakasema ' ama nyie mtende'. Kwa maana mmefanya kazi kubwa ya kilimo.Nao wakajibu "kwani nyie mjikalii makunduchi?" na hii ndiyo sababu ya kupewa jina la Mtende. Kama melezo yanavyotuonyesha, utafiti wa Masoud (keshatajwa) ulizingatia masuala ya asili ya vijiji na wakaazi wa vijiji lakini haukuchunguza jinsi majiana hayo yanavyoakisi utamaduni.

Ingram (2007) ameeleza asili ya neno Zanzibar ni ' Zinjiba' linalotokana na lugha ya Kifarsi,lenye maana ya ardhi nzuri ya watu weusi.Neno Unguja lina asili ya Kiswahili linatokana na neno 'Ungu-jaa' lenye maana ya kisiwa chenye watu wengi, vyakula tele na ibada nyingi. Kwa upande wa kisiwa cha Pemba, kinatokana na neno la Kiswahili 'kupemba' lenye maana ya kupembua ama kuongoza chombo kwa uangalifu kutokana kisiwa hiki kuwa kimezungukwa na mkondo mkubwa wa bahari. Kazi hii nayo ni muhimu kwa utafiti huu kwani zimetoa muelekeo wa kugundua asili za baadhi ya majina.

BAKIZA (2011), wametaja majina ya mitaa inayopatikana mjini unguja, sehemu alizokua akiishi mwanasanaa jadiya mashuhuri Bwana MSA. Wametaja jina la Kundemba, palikuwa maarufu kwa pombe za kienyeji na ngoma ya mbwa kachoka

(beni) pamoja na sherehe za tafrija. Baraste kpande, ulikuwa mtaa wa kukutanisha tamaduni za majumba ya mawe na ng’ambu. Kwa hivyo maelezo ya wataalamu hao walijikita zaidi na kueleza asili za mitaa lakini hawakuzingatia majina hayo yanavyoakisi utamaduni ambayo ndiyo aliyoishughulikia mtafiti wa kazi hii.

# SURA YA TATU

# MBINU ZA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Sura hii inazungumzia utaratibu na mbinu mbali mbali zilizotumika katika utafiti huu. Pia mbinu zilizotumika kuchanganua data zilizokusanywa zilijadiliwa hapa. Opie (2010) anaeleza mbinu za utafiti kuwa ni dhana au hatua za kitaalamu za kupata taarifa kwa kuzingatia njia ambazo zitapelekea kupata data za uhakika kuhusiana na utafiti unaofanyika.

## 3.2 Mpango wa Utafiti

Utafiti huu ulifanyika katika mkoa wa Kaskazini Pemba. Sehemu zilikazohusika ni wilaya ya Wete na wilaya Micheweni. Data zilikusanywa kwa njia ya udodosaji na mahojiano na uchanganuzi wa data ni wa njia ya kimaelezo na zilichanganuliwa kulingana na madhumuni na makundi yanayolingana. Pia, takwimu zilitumika katika kuweka idadi ya watifitiwa katika kufafanua maelezo yao.

## 3.3 Eneo la Utafiti

Utafiti huu ulifanyika katika maeneo ya Kaskazini Pemba ukihusisha wilaya zake zote mbili, yaani wilaya ya Wete na wilaya ya Micheweni. Wilaya ya Wete ina jumla ya shehia thelathini na mbili (32) ambazo ni Kisiwani, Junguni, Shengejuu, Chwale, Jadida, Pandani, Mzambarauni Takao, Kiuyu Minungwini, Selemu, Limbani, Bopwe, Kizimbani, Fundo, Ukunjwi, Kojani, Maziwani, Mjini Ole, Kinyikani, Pembeni, Piki, Mtambwe Kusini, Mpambani, Kipangani, Kangagani, Ole, Mchangamdogo, Kambini, Kiungoni, Mtambwe Kaskazini, Utaani, Gando na Kiuyu

Kigongoni. Wilaya ya Micheweni ina shehia za Micheweni, Msuka, Kinowe, Tumbe, Mgogoni, Shumba Viamboni, Finya, Konde, Wingwi Mapofu, Kiuyu Maziwa-Ng'ombe, Makangale, Wingwi Njuguni na Shumba Mjini.

Baadhi ya majina ya maeneo yanayopatikana katika shehia tajwa hapo juu ndiyo yaliyohusishwa katika ukusanyaji wa data za uwandani. Upendeleo katika uteuzi wa maeneo ulihusu maeneo yote yenye kuhusiana na historia pamoja na tamaduni za wanajamii. Kwa upande wa wilaya ya Wete, tulitembelea zaidi maeneo ya Mtambwe, Gando, Mchangamdogo, Pandani na Wete; na Kiuyu (M'buyuni na Maziwang'ombe), Tumbe, Wingwi, Mgogoni na Micheweni kwa upande wa wilaya ya Micheweni. Sababu ya kuchagua maeneo hayo ni kutokana na wepesi wa mtafiti wa kuyafikia maeneo hayo katika masuala ya usafiri.

## 3.4 Kundi Lengwa

Cooper (1989) na Vans (1990) wanafasili kundi lengwa kuwa ni wanachama wote, mtu mmoja, kikundi au elementi ambazo mtafiti amekusudia kuzihusisha katika utafiti wake. Hivyo katika utafiti huu kundi lengwa ni wanajamii wanaoishi katika maeneo mbalimbali ya mkoa wa Kaskazini Pemba. Kundi hili hutambuliwa kwa jina moja la *Wapemba*. Hata hivyo, *Wapemba* ni jina la jumla linalotaja watu au wanajamii wenye asili ya uzawa na/au wanaoishi katika kisiwa cha Pemba.

## 3.5 Uteuzi wa Sampuli

Sampuli ni watu, vitu au maeneo yaliyoteuliwa na mtafiti kwa niaba ya walengwa wa utafiti ili uchunguzi ufanywe kwao kwa sharti la kupata taarifa stahiki juu ya jambo linalochunguzwa. Sampuli hupatikana kutokana na mbinu anuai za usampulishaji.

Usampulishaji ni utaratibu autumiao mtafiti kupata watu, vitu au maeneo ya kuyachunguza. Ni mchakato wa kuchagua idadi maalumu ya watu au vitu kutoka katika kundi la walengwa kiasi kwamba idadi iliyoteuliwa ina viashiria wakilishi vya sifa zilizopo kwenye kundi kubwa la walengwa. Aina (mbinu) za usampulishaji kwa mujibu wa Adam na Kamuzora (2008) ziko za aina mbili (2) za msingi: Usampulishaji Welekeo na Usampulishaji Usiwo Welekeo.

Usampulishaji Welekeo ni kielelezo cha usampulishaji ambacho kinatoa fursa au nafasi kwa kila mtu, kitu, eneo, n.k kuteuliwa na kuhusishwa katika uchunguzi. Wahusika wote huwa na nafasi na haki sawa ya kuteuliwa wakati wa kutafuta uwakilishi. Aina hii haina upendeleo kwa muhusika yeyote kwa vile nafasi ya kuteuliwa inaweza kumuangukia muhusika yeyote ilimradi yumo kwenye jamii ya *Walengwa*. Katika Usampulishaji Usiwo Welekeo, uteuzi wa wawakilishi hauachwi hivihivi tu bali mtafiti huamua kwa makusudi kumteua muhusika fulani kuwa mwakilishi wa wengine. Pengine, vigezo vya uteuzi wa wawakilishi vyaweza kuwa bayana lakini si kila aliyemo kwenye jamii ya watafitiwa anaweza kuchaguliwa. Hivyo, kwa mbinu hii, upendeleo huwekwa kutegemea data alizonazo mwakilishi pamoja na mahitaji ya jambo lichunguzwalo.

Kwa kuwa si rahisi kuwahoji watu wote wanaoishi katika eneo la utafiti, mtafiti atalazimika kufanya uteuzi wa sampuli ambayo itawakilisha wengine. Hapa tulitumia aina ya usampulishaji usiwo welekeo. Katika kuteua sampuli mtafiti alizingatia zaidi uwepo wa data zinazohitajika sio tu katika kuteua maeneo bali hata katika kuteua watu wa kuwahoji na kuwadodosa. Jambo la kwanza lilihusu uteuzi wa maeneo.

Kutokana na mada na malengo ya utafiti huu, maeneo yaliyoteuliwa ni yale yanayoaminiwa kuwa na taarifa muhimu za utafiti huu. Hapa tulichagua maeneo (vijiji) 20 ambapo katika kila wilaya tuliteua vijiji 10. Uteuzi huu tuliufanya kiholela ingawaje kila eneo liliteuliwa kwa kusudio maalumu. Uteuzi wa maeneo haya ulizingatia maelekezo tuliyoyapata kutokana na taarifa za awali za watafitiwa wa kundi la kwanza kama tulivyowaeleza hapa chini wakati tukifafanua jambo la pili la usampulishaji.

Jambo la pili lilihusu uteuzi wa watafitiwa. Kutokana na aina ya taarifa zinazohitajika ili kufanikisha malengo ya utafiti huu, watafitiwa waliteuliwa kwa njia kuu mbili: Usampulishaji Wenye Makusudio na Usampulishaji wa Kimkufu. Kwanza, tutateua kundi la kwanza linalowahusisha viongozi wa serikali ambao wanahusika katika utunzaji wa taarifa za wanajamii. Hapa tutawahusisha wafanyakazi wawili katika jumba la kutunza kumbukumbu (Jumba la Makumbusho) la Chake Chake Pemba; pia masheha wa shehia zinazohusika. Kundi la pili lilihusisha wanavijiji. Uteuzi wa kundi la pili ulifanikiwa kutokana na mashirikiano na wateuliwa wa kundi la kwanza. Hivyo, idadi ya watafitiwa wa utafiti huu inaoneshwa kwa muhutasari katika jedwali hapa chini.

**Jedwali Na. 3.1: Makundi ya Watafitiwa, Maeneo Watokayo na Idadi Yao**

| **Na.** | | **Viongozi wa Serikali** | **Wanajamii** | **Jumla** |
|---|---|---|---|---|
| | Wilaya ya Wete | 5 | 20 | 25 |
| | Wilaya ya Micheweni | 5 | 20 | 25 |
| | Maeneo Mengine | 2 | - | 2 |
| **Jumla** | | **12** | **40** | **52** |

Chanzo: Mtafiti (2015)

Jedwali la hapo juu linaonesha kuwa utafiti huu utakuwa na jumla ya watafitiwa 52. Wafanyakazi wawili katika jumba la makumbusho; viongozi 10 wa serikali, 5 kutoka wilaya ya Wete na 5 kutoka wilaya ya Micheweni; na wanajamii 40, 20 kutoka katika vijiji 10 vya wilaya ya Wete ambapo katika kila kijiji tuliteua watu wawili (2) na watu ishirini (20) kutoka katika vijiji 10 vya wilaya ya Micheweni ambapo katika kila kijiji tuliteua watu wawili (2). Kwa upende wa wanakijiji, kigezo cha umri kilizingatiwa pia ambapo kipaombele chetu kilikuwa watu wenye umri wa miaka 60 au zaidi. Kwa kuwa uteuzi wetu ulikuwa na upendeleo, suala la jinsia halikuzingatiwa sana.

## 3.6 Mbinu za Kukusanya wa Data

Kothari (1990) anasema mbinu ya kukusanya data ni zoezi la awali katika utafiti ambalo humuwezesha mtafiti kupata taarifa alizozikusudia ili kumfikisha kwenye malengo yake ya utafiti. Best na Kahn (1993) wakisisitiza umuhimu wa kutumia mbinu zaidi ya moja katika kukusanya data wanasema kuwa, kila mbinu ya kukusanya data ina ubora na changamoto zake. Njia mojawapo ya kupunguza changamoto na kuongeza ubora ni kutumia mbinu zaidi ya moja katika utafiti. Hivyo katika utafiti huu mtafiti alitumia mbinu za hojaji na udodosaji. Mbinu hizi zilitumika sambamba na upitiaji wa nyaraka na kumbukumbu muhimu ili ziweze kukamilishana.

### 3.6.1 Hojaji

Hojaji au udodosaji ni mbinu ya ukusanyaji wa data ambayo mtafiti huandaa maswali yanayoelekeza namna ya kujibu na kuwapa watafitiwa ili wayajibu (Enon, 1998). Kothari (1990) yeye anasema kwamba, hojaji ni mbinu ya kukusanyia data

ambapo mtafiti huandika maswali na kisha kuyapeleka kwa watoa taarifa ili wayajibu na baadae kumrudishia mtafiti yakiwa tayari yemeshajibiwa.

Mtafiti alitumia mbinu ya hojaji ilimsaidiasana kufanya ulinganifu wa majibu yailiyopatikana kwa watafitiwa wote. Hojaji ni njia rahisi kupata taarifa kwa watafitiwa wengi kwa wakati mmoja, pia ni rahisi kufanya majumuisho ya majibu, inaokoa muda, pia husaidia kutunza siri. Mbinu hii ilitumika katika ukusanyaji wa data kutoka kwa viongozi wa serikali. Ingawa ni mbinu bora lakini pia ina changa moto zake. Miongoni mwa changamoto hizo ni kutorejeshwa nyaraka za hojaji kutoka kwa baadhi ya watafitiwa. Watafitiwa wengine hawazijibu hojaji na kusababisha ufinyu wa yale aliyoyatarajia mtafiti. Hata hivyo, jitihada ilifanywa kutatua changa moto hizi. Mtafiti alijitahidi kuwafahamisha watafitiwa juu ya umuhimu wa ushiriki wao katika ufanikishaji wa utafiti huu ili kuwapa moyo wa utoaji taarifa. Kuhusu hojaji zilizobaki kwa watafitiwa mtafiti alizifuata na kuzisimamia hadi ujazaji ukakamilika.

### 3.6.2 Mahojiano

Kwa mujibu wa Enon (1998) mahojiano ni mbinu ya kukusanya taarifa inayohusisha uulizaji wa maswali kwa njia ya ana kwa ana. Mbinu hii humwezesha mtafiti kuhoji watu binafsi au kundi maalumu kwa maswali madogo madogo yanayohusu suala lake la utafiti (Simiyu, 2011). Mahojiano haya yalifanywa kwa hali ya nusu funge, baadhi ya maswali kutayarishwa kabla ya mahojiano na mengine kutolewa na mtafiti papo kwa papo. Mbinu hii ilitumika katika ukusanyaji wa data kutoka kwa wanajamii walioko kwenye vijiji tulivyoviteua. Mbinu hii ni nzuri kwani humsaidia mtafiti kupata taarifa za ziada zitakazotolewa na watafitiwa baada ya kuwauliza

maswali ya ziada jambo ambalo sio rahisi kupatikana katika mbinu ya hojaji. Pia ilimsaidia mtafiti kupata mawazo na mitazamo ya watafitiwa kuhusu asili ya anachokichunguza. Tatizo la mbinu hii ni kuwa mtafiti anaweza kukosa taarifa muhimu na sahihi kwani watafitiwa huogopa kuhojiwa kutokana na aibu au vitisho katika jamii. Pia, isipodhibitiwa vyema, inaweza kutoa majibu yasiyohitajika kwa kuwa mtafitiwa anaweza kujieleza na kueleza jambo aliloulizwa kwa kina zaidi. Hata hivyo, umakini mkubwa uliwekwa wakati wa mahojiano na watafitiwa watahakikishiwa kuwa taarifa zao ni siri baina yao na mtafiti na zitatumika kwa ajili ya utahini na uandaaji wa kazi hii tu.

## 3.7 Vifaa vya Utafiti

Vifaa vya utafiti ni vyombo ambavyo mtafiti huvitumia katika ukusanyaji wake wa data (Kothari, 2009). Mtafiti anatarajia kutumia vifaa vifuatavyo; alitumia Tarakilishi: Mtafiti atatumia tarakilishi kwa ajili ya kuwekea kumbukumbu za utafiti. Ngamizi nakilishwa.diski tembezi kwa ajili ya kucharaza na kuhifadhi taarifa.

## 3.8 Uchambuzi wa Data

Data zilichambuliwa kwa njia ya maelezo. Nadharia jumuishi ilitumika ili kupima maswali ya utafiti huu. Data hizo zilifasiriwa ili kutoa tafsiri sahihi ya kilichowakilishwa kutegemeana na malengo yaliyowekwa. Data ilifafanuliwa kulingana na malengo ya utafiti.

### 3.8.1 Maadili ya Utafiti

Kwa mujibu wa Sture (2010) mkabala wa maadili ni moja miongoni mwa masuala muhimu ambayo mtafiti anapaswa kuyazingatia kwa uzito kwa uzito mkubwa wakati

akifikiria, akipanga, kutekeleza na hata baada ya kukamilisha utafiti wake. Adam na Kamuzora (2008) wametaja maadili ya utafiti kuwa ni haki ya kuwa na siri, yaani mtafiti hatatoa siri za mtafitiwa. Pia anasema haki ya mtafitiwa kuhakikishiwa usalama wake, haki ya kujua madhumuni, haki ya kupata matokeo ya utafiti, haki ya kujibu swali atakalopenda kujibu na haki ya kukataa kushiriki kwenye utafiti. Mtafiti alitambua haki zote hizi na kuzifanyia kazi, kwani utafiti huu ulizingatia misingi yote ya utafiti ikiwa ni pamoja na kupata ridhaa ya wahojiwa ingawa taarifa za utafiti huu zisengeleta madhara yeyote.

## 3.9 Hitimisho la Sura

Sura hii ilieleza kwa kiasi mbinu zilizotumika katika utafiti huu, mpango wa utafiti, eneo la uatfiti sampuli na usamplishaji mbinu za kukusanyia data na maadili ya utafiti.

# SURA YA NNE

# UCHAMBUZI WA DATA

## 4.1 Utangulizi

Katika sura hii, mtafiti ameziwasilisha data zilizokusanywa kutoka uwandani. Uchambuzi huu umezingatia mambo matatu makubwa na muhimu. Jambo la kwanza, mtafiti amechambua na kuchanganua data zake kwa kuzingatia malengo na mswali ya utafiti aliyoyadhihirisha kwenye (1.4.2). Jambo la pili, uchambuzi na uchanganuzi wake umezingatia kiunzi cha nadharia alichokipendekeza kwenye (2.6). Na jambo la tatu, amewasilisha uchambuzi wa data zake kwa kufuata njia za uchambuzi wa data alizobainisha kuwa atazitumia kama alivyoonesha kwenye (3.7).

## 4.2 Kubainisha Majina ya Mahali ya Kaskazini Pemba

Mtafiti alikusanya data inayohusu majina ya mahali kutoka katika maeneo yaliyoteuliwa. Mbinu alizozitumia kukusanya data hizo ni mahojiano na dodoso. Mbinu hizo zimemuwezesha mtafiti kuweza kupata data zinazoonesha uhalisia unaoonesha kuwepo kwa majina ya mahali yanayoakisi matukio ya kihistoria katika baadhi ya maeneo ya Kaskazini Pemba. Utafiti umeonesha kwamba kila mtaa au kijiji kiliitwa kwa jina linalotambulisha sehemu kwa asili yake kihistoria na kiutamaduni.

Ni dhahiri kuwa, kila kitu kina chanzo na asili ya kuwepo kwake, na kwa hivyo majina ya mahali yana asili yake kama wataalamu mbali mbali walivyolieleza na kulifafanua jambo hilo. Kwa mfano Tolmacheva (1993), alieleza etimolojia ya mji wa Siu Mombasa na akaibuka na maoni yasemayo kwamba, asili ya mji huu kuitwa

Siu ni watu ambao walikimbia vita vya Pate na majirani zao. Watu hawa wakahalifu kupigana na wakakimbia. Zilipita siku ndipo walipoonekana wakarudishwa na mfalme wa Pate na ndio wakarudi mjini pao na pakaitwa kwa jina la Siu.

Maelezo hayo yanaonesha ukweli kwamba wataalamu walitafiti majina ya sehemu na kila mtaalamu alikuwa na vigezo alivyovitumia ili kugundua asili ya vijiji kihistoria na kiutamaduni. Watafitiwa wa kazi hii huko uwandani, walitoa maelezo yanayohusiana na asili ya vijiji mbalimbali. Kila mtafitiwa aliyeteuliwa alitakiwa aeleze asili ya sehemu anayoishi yeye mwenyewe. Watafitiwa walitowa maelezo yaliyomsaidia mtafiti kuweza kufikia uchambuzi unaoakisi malengo yake ya utafiti aliyoyakusudia.

#### 4.2.1 Etimolojia ya Jina la Mji wa Wete

Wete ni mmoja miongoni mwa miji mitatu mikuu iliyoko kisiwani Pemba. Huu ndio mji mkuu wa mkoa wa Kaskazini Pemba. Mji huu upo katika wilaya ya Wete, Mkoa wa Kaskazini Pemba. Kwa upande wa Magharibi mji huu umepakana na bahari ya Hindi, ambapo upande huu yapata kilomita 12 kutoka bandarini kunapatikana visiwa kadhaa vinavyoishi au kukaliwa na watu. Miongoni mwa visiwa hivyo ni Fundo, Funzi na Uvinje. Kwa upande wa Kaskazini mji huu umepakana na vijiji vya Gando,

Ukunjwi na Taifu, ihali kwa upande wa Mashariki Wete imepakana na kijiji cha Pandani kwa upande mmoja na kijiji cha Finya kwa upande wa pili. Kusini Mashariki ya Wete kuna kijiji cha Mzambarau Takao na Kusini Magharibi kuna Piki na Mtambwe. Wete ni mji wa bandari ambapo ndipo panaposemekana kwamba wakoloni wa Kireno walifikia. Yasemekana kuwa, Wareno waliuita mji huu kwa

jina la Weti na baadae jina hilo likabadilika kuwa *Wete*, kwa maana ya waite watu kutoka sehemu nyegine za ndani ya Pemba waje waangalie maendeleo yaliyopatikana kwa haraka katika mji huu. Wapo waonao kwamba *Wete* asili yake ni ya Kibantu, iliyotokana na mabadiliko ya kimofofonolojia ambayo imefuata kanuni ya mvutano wa irabu, ambao kwa muhtasari unaweza kuwasilishwa kwa kanuni, ***/Waite/→Wete; /a+i/→ɛ́***

Kwa ujumla tunaewza kusema kwamba kuna hitilafu juu ya asili ya jina la Wete. Wapo waonao kwamba, jina hili lililetwa na Wareno, na wapo waonao kwamba, jina linatokana na Wabantu wenyewe, kupitia kanuni za kifonolojia. Katika hali zote mbili jina lilikuwa na lengo la kutoa agizo la kuwataka watu wengine waje kwenye mji huu kuangalia maendeleo yaliyofikiwa na Wareno.

### 4.2.2 Etimolojia ya Jina la Kijiji cha Chasasa

*Chasasa* ni mtaa miongoni mwa mitaa mashuhuri iliyo ndani ya mji wa Wete. Chasasa ni mtaa ambao upo upande wa juu; kando kidogo ya mji wa Wete. Mtaa huu umejitenga upande wa Kusini Mashariki, yapata kilomita mbili na nusu Kusini Mashariki ya mji wa Wete. Mtaa wa *Chasasa* umepakana na kijiji cha Mkwajuni kwa upande wa Mashariki, kimepakana na mtaa wa Utaani na Mtemani kwa upande wa Kaskazini na kimepakana na kijiji cha Limbani kwa upande wa magahribi.

Mtaa huu ulianzishwa kwa ajili ya kuupanua mji wa Wete na kutoa makazi mapya ya watu. Na kwa kuwa majengo yaliyokuwepo yalitofautiana na yale ya Wete kwa ubora na mpangilio, mtaa huo ukapata jina kuwa ni “kijiji cha sasa”, na kwa hivyo ukaitwa “*Chasasa.”* Kwa ufupi mtaa huu uliitwa *Chasasa* kwa kuwa yalikuwa ni

makazi mapya ya Wete yaliyokuwa na mpangilio wa kisasa kwa mintarafu ya wakati huo.

### 4.2.3 Etimolojia ya Jina la Kijiji cha Jadida

Watu wa asili ya Kihindi na Kiarabu walijitenga na kujitofautisha na raia wenye asili ya Kiafrika kimakazi. Pembezoni kidogo mwa mji wa Wete na Magharibi ya mtaa wa Utaani na Chasasa mtaa mwingine kwa ajili ya Wahindi na Waarabu ulianzishwa. Jamii hizi mbili ziliamua kujenga shule maalumu kwa ajili ya kusomeshea watoto wao bila kuruhusu mchanganyiko na watoto wa makabila mengine. Shule hii ilijulikana kwa jina la shule ya Jadidah yaani shule mpya. Jadidah ni neno la lugha ya Kiarabu lenye maana ya '***mpya***'. Mtaa huu ukapewa jina kutokana na jina la shule hii; Jadidah. Awali mtaa huu ulikuwa ukijulikana kwa jina la Mshelsheli Kibutu kwa maana ya kuwa palikuwa na mshelisheli uliokatwa sehemu yake ya juu na kuachwa ukiwa butu; bila matawi. Upande wa Kusini *Jadidah* imepakana na mtaa uitwao Mji mwema. Magharibi ya Jadidah kuna mtaa uitwao Bubujiko na Kaskazini yake kuna mtaa wa Mtemani, sehemu iliyojengwa nyumba za maendeleo na Raisi wa kwanza wa Zanzibar huru Bwana Abeid Amani Karume. Kwa ufupi mtaa huu uliitwa *Jadidah* kwa sababu ni mtaa ulokuwa mpya ulioanzishwa na watu wa mbegu nyeupe; Wahindi na Waarabu.

### 4.2.4 Etimolojia ya Jina la Mtaa wa Mtemani

Mtaa huu upo karibu na mji wa Wete, kama kilomita moja kuotka bandarini. Uko upande wa Kusini Mashariki ya Bandari ya Wete, Upande wake wa Mashariki kuna mtaa wa Utaani na Kusini kuna Jadidah kama ilivyokwisha kuelezwa na mtafiti kwenye **(**4.2.3**)**. Upande wake wa Kaskazini kuna mtaa wa Bopwe. Inasemekana

kwamba, katika miaka ya utawala wa mfalme wa jadi, aliyekuwa akiishi kwenye eneo la Mtambwe, *Mtemani* palikuwa pori ambalo mfalme huyo alituma watu wake kulitema yaani kulifyeka ili kutayarisha eneo maalumu kwa ajili ya kilimo. Kwa muktadha huo, eneo hilo likapewa jina la *Mtemani*, yaani mahali palipotemwa. Watu waliokuwa wakitoka Mtambwe kuja eneo hilo kwa ajili ya kilimo, walikuwa wakisema wanakwenda *Mtemani.* Jina hilo likabaki na likawa ndio jina la mtaa huo, tangu nyakati hizo hadi sasa. Kwa ufupi mtaa huu uliitwa *Mtemani* kwa kuwa palitemwa na wafuasi wa mfalme wa Jadi kwa matayarisho ya kilimo.

### 4.2.5 Etimolojia ya Jina la Mtaa wa Miti Ulaya

*Miti ulaya* ni mmoja kati ya mitaa iliyopo katikati ya mji wa Wete ambapo katika utawala wa Wareno ndipo ilipopitishwa barabara kuu iliyounganisha mtaa huu na mitaa mingine ya mji wa Wete. Miti ya kivuli ambayo hutoa maua kila ufikapo mwezi wa Disemba iitwayo ***'Christmas tree'*** ilipandwa katika eneo hili. Miti hii mpaka leo hii ipo kwenye eneo hilo. Wakazi wa Wete wa wakati huo, waliamini kwamba miti hiyo ilitoka Ulaya, na wakaiita miti ulaya. Mtaa huo kwa hivyo nao ukaitwa mtaa wa Miti ulaya.

Jina hilo lilidumu na limeendelea kutumika hadi leo. *Miti ulaya* ni mtaa wa bandari na kwa hivyo umepakana na bahari ya Hindi kwa upande wa Magharibi, upande wa Mashariki umepakana na mtaa uitwa Selemu ulio katikati ya mji wa Wete. Kusini ya Miti Ulaya kuna eneo liitwalo Machinjioni na Kaskazini kuna mtaa uitwao Majimbikani. Maelezo hayo yanaonesha kwamba, mtaa wa *Miti ulaya* umepata jina lake kutokana na kuwepo miti iliyopandwa kwenye mtaa huo, iliyoitwa na wenyeji wa Wete kuwa miti ulaya, kutokana na asili ya miti hiyo.

### 4.2.6 Etimolojia ya Jina la Mtaa wa Uzunguni

Mtaa wa *Uzunguni* ni katika mitaa mikongwe na mitaa anzilishi ya mji wa Wete. Mtaa huu upo juu ya kilima njiani kuelekea bandarini. Mtaa huu ulipewa jina la *Uzunguni* kwa sababu ndipo yalipoasisiwa makazi waliyoishi wafanya kazi wa Serekali wakiwemo polisi, madaktari, mahakimu, makarani na maafisa wengine ambao wengi wao walikua ni Wazungu. *Uzunguni* ni eneo ambalo mpaka leo majengo makongwe yenye athari ya enzi za kale yanapatikana na yale yaliyokuwa hayajabomoka yanatumika kama ofisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. *Uzunguni* imepakana na mtaa wa Kipangani bondeni kwa upande wa Kusini, umepakana na mtaa Kilima ndege kwa upande wa Kaskazini, umepakana na mtaawa Mbuyuni. upande wa Magharibi ilhali Mashariki yake kuna mtaa wa Magereza. Kwa ujumla mtaa huu uliitwa *Uzunguni* kwa sababu ya makazi ya wafanya kazi waliokuwa wakiishi hapo ambao wengi wao walikuwa ni Wazungu.

### 4.2.7 Etimolojia ya Jina la Mtaa wa Kilimandege

*Kilima ndege* ni kilima amabacho kipo katikati ya mji wa Wete ampo njia kuu kutoka bandarini inapata kwenda sehemu mbali mbali za kisiwa cha Pemba. Kilima hiki kimeitwa *Kilimandege* kwa sababu hapo zamani palikuwa na miti mingi na mikubwa ambapo ndege wa aina mbalimbali walikuwa wakipunga upepo kwenye eneo hilo. Walikuwa wakidondoa wadudu na kufyonza maua kwa ajili ya kujikimu kwa shida ya njaa. Ndege hao walikuwa wakibaki kwenye eneo hilo takriban muda wa mchana mzima. Kwa kuwa eneo hili lilikuwa juu ya Kilima na kwa kuwa palikuwa ni mahali pa mapumziko ya ndege, jina la *Kilimandege* lilibuniwa na likadumu kwa muda na dahari na hadi leo linaendelea. *Kilimandege* ni mtaa

uliopakana na mtaa wa Sebuwatu kwa upande wa Kaskazini, Kusini yake kuna kipangani juu, Magharibi kuna Selemu na Mashariki kuna Mtemani. Kwa ufupi mtaa huu umeitwa kilima ndege kwa kuwa, ni sehemu iliyo juu ya kilima na iliyokuwa mapumziko ya ndege kabla miti mikubwa haijakatwa na mazingira ya eneo hilo kugeuzwa makazi ya watu.

### 4.2.8 Etimolojia ya Jina la Mtaa wa Sebuwatu

*Sebuwatu* ni mtaa ulio katika mji wa Wete. Mtaa huo uko pembezoni kidogo ya mji huo. Kusini yake kama mtafiti alivyoashiria kwenye (4.1.7) kuna mtaa wa Kilimandege, Kaskazini yake kuna maeneo ya kilimo cha mazao mbalimbali, Mashariki ya Sebuwatu kuna mtaa wa Bopwe ilhali Magharibi yake kuna mtaa wa Kibokoni. Bwana-Khamis Masoud (60) miongoni mwa watafitiwa ambaye alihojiwa anaeleza kwamba, mwanzilishi wa mtaa huo, alikuwa ni mtu aliependa kuishi peke yake. Aliishi juu ya kilima sehemu iliyokuwa imejitenga na mji kwa wakati huo. Kwa kweli sehemu hiyo ilikuwa nje ya mji wa Wete. Mtu huyo alichukua eneo kubwa akaliweka chini ya milki yake.

Katika eneo hilo alipanda miti ya mikarafuu na kwa kweli aliwapiga marufuku watu na kuwataka wasiingie huko bila ya idhini yake. Alitangaza waziwazi kwamba hataki watu watembelee eneo hilo bila ya kuwa na shughuli inayomuhusu yeye au familia yake. Kutokana na muktadha huo eneo hilo likaitwa *Sebuwatu*. Neno sebu maana'ake ***sitaki*** kwa hivyo *Sebuwatu* maana yake sitaki watu. Kwa kifupi, *Sebuwatu* ni jina lililotokana na histori ya mmiliki wa eneo hilo, ambae kwa kweli alikuwa hataki watu waingie kwenye eneo lake. Na kwa hakika alikuwa akisema wazi wazi kwamba sitaki watu yaani *Sebuwatu.*

#### 4.2.9 Etimolojia ya Jina la Mtaa wa Majimibikani

*Majimbikani* ni mtaa ambao uko Kaskazini mwa Mtaa wa Miti Ulaya, Magharibi kuna Sebuwatu. Kwa upande wa Kusini Mashariki kuna mtaa wa Selemu. Kabla ya kuwa mtaa, eneo hilo lilikuwa na miti mingi sana, hasahasa miti ya miembe na mishelisheli. Kwa wingi wa miembe na mishelisheli, sehemu hii ilikuwa na vivuli vya kutosha kulikoifanya ardhi ya hapo kuwa na rutba ya kutosha kwa ajili ya kuotesha mazao ya aina mbalimbali. Zao kuu lililostawishwa eneo hilo ni majimbi (majimbi ni aina ya viazi vinavyopendwa sana kisiwani Pemba. Ni viazi vyenye bei kubwa zaidi hata kuliko viazi vitamu na viazi tona). kwa hivyo watu waliokuwa wakienda kuchimba majimbi kwa ajili ya chakula walipaita mahali hapo kuwa ni *Majimbikani.* Kwa ufupi mtaa wa *Majimbikani* ulipata jina lake hilo kwa sababu ya zao la viazi majimbi lililokuwa likilimwa eneo hilo.

#### 4.2.10 Etimolojia ya Jina la Mtaa wa Maskini Hajengi

Mtaa huu si wa zamani sana, umepata jina lake hivi karibuni. Mtaa huu upo Kusini ya Chasasa, Magharibi ya Mkwajuni, Mashariki ya Limbani, Kaskazini ya mtaa uitwao Kilimo. Mtaa huu ulipendwa sana na watu wa tabaka la wenye kipato cha juu; matajiri. Matajiri wengi walijenga majumba ya fahari katika eneo hilo.Walimilki maeneo makubwa makubwa ya ardhi ili kuzizunguuishia mageti nyumba zao.

Inasemekana kwamba tajiri mmoja alinunua nyumba ya maskini iliyokuwa karibu na kiwanja chake. Maskini huyo alilazimika kuiuza nyumba yake na kwenda kujitafutia kiwanja eneo jengine nje ya mtaa huo. Watu walipo lishuhudia jambo hilo wakasema kwamba, maskini hajengi tena katika mtaa huu. Kwa sababu hiyo, jina la mtaa huu likawa *Masikini hajengi*. Kwa ufupi, mtaa huu uliitwa *Maskini hajengi* kwa

sababu ya kuhamiwa na matajiri waliojenga majumba makubwa makubwa yaliyowalazimisha maskini kuuza majumba na ardhi zao kupisha wahamiaji wa wenye kipato.

### 4.2.11 Etimolojia ya Jina la Mtaa wa Mharitani

Mharita ni mti ambao huzaa tunda ambazo hutowa povu jingi sana mithili ya sabuni. Mtaa wa *Mharitani* upo kati kati ya mtaa wa Bopwe na umepakana na viunga vya mji huo. Katika enzi za kale, tunda hizi zilikuwa zikitumika kufulia nguo na kuchukua nafasi ya sabuni hasa kwa watu masikini na wa kipato cha chini. Kwa hivyo, mtaa huu uliitwa *Mharitani* kwa kuwa eneo hilo lilikuwa na mharita mkubwa, uliokuwa ukitembelewa na watu wengi waliokwenda kujichumia harita kwa ajili ya kufulia nguo zao. Kwa hivyo, tunaweza kusema kwamba, *Mharitani* ni mtaa uliojipatia jina lake kutokana na sababu za kuwepo mharita katika zama za kale.

### 4.2.12 Etimolojia ya Majina ya Mtaa wa Kwasetimende

Setimende ni jina la mtu aliyekuwa na asili ya Kihindi. Bwana huyu alikuwa na gereji kubwa ya kutengenezea magari na vyombo vyengine vya moto. Jirani na gereji ya Setimende palikuwa machinjio ya wanyama kama ng’ombe, mbuzi, kondoo na wanyama wengine waliokuwa wakiliwa na wenyeji na wakazi wa Pemba. Jengo hilo lenye machinjio lilikuwa likimilikiwa na Serikali ya kikoloni. Kwa kuwa eneo hilo lilikuwa ni jirani ya gereji ya fundi Setimende lilipokea jina la *Kwasetimende.* Mtaa wa Kwasetimende umepakana na mtaa wa Mtemani kwa upande wa Kusini, mtaa wa-Kipangani upande wa Kaskazini, Magharibi yake kuna mtaa wa Kibokoni na Mashariki kuna mtaa waKilima hewa. Kwa ufupi jina la *Kwasetimende* lilkuja kutokana na fundi wa magari aliyekuwa akifanya kazi hapo aliyeitwa Setimende.

### 4.2.13 Etimolojia ya Jina la Mtaa wa Tangi la Maji

Mtaa wa *Tangi la maji* upo kwenye mapishano ya njia inayoelekea Gando kwa upande mmoja na Konde kwa upande wa pili. Katika eneo hili, palikuwa na Tangi kubwa la kuhifadhia maji yaliyopelekwa kwenye sehemu mbali mbali za mji wa Wete kwa matumizi ya wakazi wake. Kutokana na sababu hiyo mtaa huu ukaitwa *Tangi la maji*. Jina hili linaendelea mpaka leo ingawa hilo Tangi la asili halipo tena. Sasa hivi lipo tangi lenye muundo mwingine kinyume na ule wa zamani. Kwa ufupi mtaa huu uliitwa *Tangi la maji* kutokana na historia ya kuwepo Tangi la maji katika enzi za wakoloni.

### 4.2.14 Etimolojia ya Jina la Eneo la Kishukashi

Hii ni sehemu ya pwani, pembeni kidogo ya bandari ya Wete kwa upande wa Kaskazini Magharibi. Kwa mujibu wa Bwana Moh'd Salim, aliyehojiwa na mtafiti tarehe —17 Aprili, katika enzi za utawala wa Kiarabu, mtawala mmoja wa Kiarabu aliingia Pemba kwa kutumia usafiri wa jahazi. Kwa bahati mbaya jahazi lake lilifunga nanga mbali na ufukwe na kwa hivyo ikamlazimu yeye na watu wake, wapandishe nguo zao juu ili kuepusha kuzirowesha nguo hizo kwa maji ya bahari. Wakatembea kuelekea ufukweni hali ya kuwa wamepandisha nguo mpaka sehemu za mapajani. Watu wa eneo hilo, wakawa wanaambizana kwamba, Mwarabu kashuka kutoka kwenye jahazi akiwa uchi. Walisema hivyo kwa sababu, sehemu ya juu ya magoti na mapaja yalikuwa wazi na kwa hiyo, ikasemwa kwamba Mwarabu kashuka uchi na jina la mahali hapo likawa *Kishukashi.* Wapemba hutumia neno ushi badala ya uchi. Eneo hilo kwa sasa halikaliwi tena na watu; ni eneo linalotumika kwa kilimo. Kwa mantiki hiyo, jina la mahali hapa lilitokana na tukio la mgeni

aliyeteremka kutoka kwenye jahazi akiwa anatembea nguo amezipandisha kidogo kuepuka kuroa maji na wenyeji wakasema kashuka ushi.

### 4.2.15 Etimolojia ya Jina la Kijiji cha Misooni

Huu ni mtaaa uliopo katika shehia ya Junguni Wilaya ya Wete, Kaskazini Magharibi ya mji wa Wete. Pahala hapa palikuwa na miti inayotambaa na kushikana yenyewe kwa yenyewe bila kuruhusu miti ya aina nyengie kuota baina yao. Miti hii inakuwa na miba mikali sana. Miti hii inajulikana kwa jina la misoo dume. Watu walifyeka miti hiyo kwa taabu kubwa na mashaka ya hali ya juu ili kuanzisha makazi yao. Pahala hapa pakaitwa *Misooni.* Kwa ufupi eneo hili liliitwa *Misooni* kutokana na historia ya kuwepo miti iitwayo misoo.

### 4.2.16 Etimolojia ya Jina la Mtaa wa Mjimwema

Mtaa huu ni kati ya mitaa iliyo ng'ambu ya mji wa Wete. Pahala hapa ni patulivu sana; hapana harakati za kimji. Ni mtaa ambao hata, vipando vya moto havipiti mara kwa mara maana hakuna barabara zinazounganisha mtaa huu na sehemu nyengine. Barabara iliyoko huko ni ya kuingilia na kutokea tu. Watu waliojenga na kuhamia huko ni watu wema, watulivu na wenye kujitosheleza kimaisha, wengi wao wamezungushia kuta majumba yao na kwa hivyo wana usalama wa maisha yao, watoto na mali zao. Hali ya hewa ya eneo hil ni nzuri. Ni eneo lenye upepo mwanana hasa katika nyakati za jioni. Ni mtaa mwema wa kuishi. Na kwa hali hiyo watu wa Wete, hasa wanaoishi jirani na mtaa huo waliuita *Mji mwema.* Kiufupi jina la *Mjimwema* lilitokana na historia ya wakazi wake.Kutokana na hali ya utulivu waliokuwa nao na eneo lenyewe kuwa kimya na salama.

### 4.2.17 Etimolojia ya Jina la Kijiji cha Madenjani

Mtaa huu upo pahala ambapo barabara kutoka Wete kwenda Chake hukutana na barabara kutoka Konde kwenda Chake. Wenyenji wa mtaa huu wanatamani pangeliwekwa yale mataa ya kuogozea magari ambayo waliyaita madenja kwa hivyo sehemu ikapata jina la *Madenjani* yaani pahala penye mataa ya kuongozea magari barabarani.

### 4.2.18 Etimolojia ya Jina la Kijiji cha Kambini

Kihistoria eneo hili lilikuwa na nyumba maalumu ya ibada (msikiti), ambapo watu wengi walikuwa wakitoka maeneo tofauti kwa ajili ya kuja kuabudu. Walikuwa wakitumia punda kama vyombo vyao vya usafiri. Walikuwa wakikutana eneo hilo na kufunga kambi kwa muda huku wakitekeleza shughuli zao za ibada. Kwa sababu hiyo sehemu hii ikaitwa *Kambini.*

### 4.2.19 Etimolojia ya Jina la Kijiji cha Gombeume

Kwa mujibu wa mtafitiwa bwana Hamad Bakari, (66) aliyehojiwa na mtafiti wa kazi hii (munamo february, 2015) asili ya hapa ni makazi ya watu wa kabila la Wagunya kutoka Mombasa jina hili ni la shetani kutokana na imani za jadi ya watu hao, ambalo wame lihamisha kutoka kwao na kulileta hapa. Lakini wahojiwa wengine alisema jina hili linatokana na mchezo wa ng'ombe ambao ulihusisha ng'ombe dume aliyekuwa akitumika katika mchezo huo. Na kwa mantiki hiyo wanajamii wakapaita *Gombeume*.

### 4.2.20 Etimolojia ya Jina la Kijiji cha Micheweni

Ni sehemu iliyoko Kaskazini Pemba katika wilaya ya Micheweni. Eneo hili lina asili ya wakazi ambao walitoka sehemu za Mombasa. Watu hawa walikuja kwa shughuli

za kibiashara, kilimo na uvuvi. Watu hawa walijinasibisha na ushirikina pamoja na kufanyiana uchawi na mambo mengine ya kikatili na ndio wanajamii wakawa na woga wakienda mahala hapo na ndio sababu ya kuitwa michawini. Kutokana na kutamkwa sana jina likabadilika kutokana na mazingira yanavyoakisi utamkaji likatamkwa *Micheweni* .

### 4.2.21 Etimolojia ya Jina la Kijiji cha Kiuyu M'buyuni

Nalo ni jina la mahali ambalo limetokana na watu hao waliokuja Micheweni. Wakazi hawa walingia kijiji hiki kwa kutumia mitumbwi wakitokea sehemu za lamu, Mombasa na Kenya walishuka sehemu ambayo ni ufukweni. Katika ujio huu walifungasha vyakula na wanyama kama mbuzi na walipofika hapo waliteremka na mbuzi wao kutafuta majani. na pakukaa kupumzika na safari. Kutokana na sehemu hii ilikua na mawe walisogea juu kidogo na kuanza maisha hapo mwenzao mmoja akisema yeye akaondoka akatafuta pengine akakaa. Lakini huko alikokwenda kukamshinda akaamua kurudi hivyo wale wenzake walipomuona wakasema kile kibibi kiuyu kwa maana kimerudi Neno "uya" lina maana ya kurejea ndio asili na chanzo cha jina hili la *Kiuyu.*

### 4.2.22 Etimolojia ya Jina la Kijiji cha Maziwa ng'ombe

Kijiji cha *Maziwang'omb*e kiko wilaya ya Micheweni kwa maelezo ya wahojiwa wa eneo hili wanasema watu wa mwazo waliokuja walijigawa kundi moja likakaa Micheweni kundi la pili likakaa kiuyu na kundi la tatu ndio hili la wafugaji na wavuvi waliokuja hapa *Maziwang'ombe.* Sababu hasa ya jina hili ni kutokana na watu waliokuwepo zamani wakifuga ng'ombe na wakawa wanakamua maziwa.

Maziwa hayo yalikua hayana kiasi kwa wingi wake watu kutoka maeneo yote takriban ya Kaskazini wakija kupata maziwa bure, pia wagonjwa wenye safura hupelekwa na kukaa hapo wiki tu hupata afya yao. Kutokana na wingi wa maziwa haya yalifika siku yakikosa wa kuyatumia yakimwagwa kwenye "mapuji" wanasema ni sehemu kama mabakuli ni mawe yaliyo na umbile la mabakuli huyamwaga humo. Hii ndio sababu na chanzo cha kuitwa jina hilo. Kijiji hiki sasa ni kame na ufgaji umekua ni mdogo sana shuguli zao sasa ni kilimo cha mwani.

### 4.2.23 Etimolojia ya Jina la Kijiji cha Chamboni

Ni kijiji ambacho kimetokana na mji wa Micheweni kijiji hiki kiko Magharibi ya mji huu wa Micheweni. Kiambo kwa maana ya sehemu iliyo pembeni mwa ule mji yaani vitongoji. Sehemu hii ilikua haikaliwi na watu ni mashamba tu kutokana na harakati za maisha na kuongezeka kwa watu, makazi mapya yalihitajika. Wenyeji wa Micheweni wakaanza kuingia kiamboni na kuanza kufyeka misitu watu wakajenga. Umbali kidogo uliokuepo na mji mtu anapoulizwa unaelekea wapi husema naenda kule kiamboni. Kutokana na lafudhi yao walipaita *Kyamboni* na hii ndio asili ya kuitwa jina hilo kwa sababu ni kiyamboni ikatamkwa *Chamboni.*

### 4.2.24 Etimolojia ya Jina la Kijiji cha Mbuyugowe

*Mbuyugowe* ni moja ya kijiji kilichopo Maziwang'ombe wakazi wake ni jamii ya watu wa palepale Maziwa ng'ombe. Walianzisha makazi hayo kwa kuongezeka kwa watu na kuanza maisha mapya. Jamii ya wakazi wa hapa wakawa na tabia ya ugomvi. Mbuyugowe ni sehemu ambayo pana mbuyu na watu waliohamia hapo walikuwa wanatabia ya kugombana wenyeji wakapaita *Mbuyugowe* lenye maana ya pahali pa ugomvi na mtu aliyekuwa hapendi ugomvi hapo hakai kwani watu wake

wote ni wagomvi. Hapa inadhihirisha kuwa jamiilugha huwatambulisha wanajamii kuwa wao ni kundi fulani na wakawa wanatumia lugha yao kwa kuelewana wanajamiilugha hao kama inavyoeleza nadharia ya Gilles.

### 4.2.25 Etimolojia ya Jina la Kijiji cha Kibagoni

Kijiji cha *Kibagoni* kiko Kaskazini Mashariki mwa Maziwang'ombe. Asili ya kijiji hiki palikua ni sehemu wanajamii wakikaa na kuzungumza bila ya kazi yoyote. Watu hutoka majumbani na kupiga gumzo katika sehemu hii. Baada ya tabia ya watu kukaa hapa kuzoeleka, watu wakapaita *Kibagoni* na ikawa kijiji kilicho na wkaazi wengi. Kwa mujibu wa maelezo ya mwanajamii wa hapo bi Uvuno, alisema watu hapo walikua wakikaa wakifuga uvivu hawendi kufanya kazi wakaa wakingoja wake zao wahangaike wao wametulia. Neno kibago alisema maana yake pahali pakukaa pa mazungumzo.

### 4.2.26 Etimolojia ya Jina la Kijiji cha Mchangamdogo

*Mchangamdogo* ni kijiji kilichoko Mashariki ya mji wa Wete, kimepakana na kijiji cha Kairo upande wa Magharibi. Kutokana na utafiti uliofanyika kijiji hiki kina asili ya watu ambao zamani walikua wana utamaduni wa kusaidiana katika shughuli mbali mbali za jamii. Mambo hayo hufanyika katika sehemu maalumu ambayo hukutana na kupeana habari. Mtu wa mwanzo aliyekaa hapo aliitwa Bimwanajuma wa Juma. Siku moja bibi mmoja alinadi jamani mchango mdogo, mkubwa mdogo muembeni kwa bintoto. Ndio jina hilo lilipoanza na kuitwa *Mchanga mdogo*. Kwa sasa *Mchangamdogo* imekua na wakazi wengi wamesogea karibu na barabara kuu kiasi ambacho unaweza kusema ni vijiji tofauti.

#### 4.2.27 Etimolojia ya Jina la Kijiji cha Wingwi Mapofu

Asili ya kijiji hiki kwa maelezo ya mtafitiwa Ali Hamad sheha wa shehia ya Wingwi njuguni alisema palikuwa na minazi mingi ambayo huzalisha nazi nhyigi katika kijiji hikcho. Katika kuvuna zao hilo la nazi, wanajamii hao walibaini kuna mnazi mmoja huo ukizaa nazi tele lakini nazi zake hazikuwa nazi watu wakichuma nazi hizo zote ni pofu. Nazi hizo kila siku hazina maana ni madude matupu hazina kitu ndani haziwezi kupikiwa. Jina hili linatokana na hizo nazi amabzo ukiziona utasema zimeongoka kumbe si nazi ni mapofu.

#### 4.2.28 Etimolojia ya Jina la Kijiji cha Tumbe

Tumbe ni miongoni mwa Miji inayopatikana katika Kisiwa cha Pemba. Mji huu una historia ndefu katika jamii ya Wapemba. Jambo hilo linatokana na Utamaduni uliopo eneo hilo, miongoni mwa mambo hayo ni mchezo wa ng`ombe, mashindano ya ngalawa na maeneo ya kihistoria ya magofu hasa ya Msikiti Chooko. Mambo hayo yameipatia Mji wa Tumbe sifa kubwa na hitoria isiyoweza kufutika. Jambo jengine ni Bandari. Hii hutumiwa na watu kutoka sehemu mbalimbali za Pemba kama vile Mkoani, Chake Chake, Wete na maeneo mengine ya Micheweni. Kihistoria mji huu unatokana na wazee wa zamani wa Tumbe na umepewa jina hilo na wazee hao. Wazee hao walitokea sehemu za Mombasa, Lamu ambao walikuja kibiashara, uvuvi na kilimo cha chooko, mtama,maharage. Watu hawa walihamia Chwaka Tumbe ambapo waliishi chini ya utawala wa Haroun kutoka Mombasa nchini Kenya. Kwa mujibu wa mahojiano na matafitiwa Mwalim Shehe Bakar wa Tumbe, watu wa mji wa tumbe walitoka Chwaka baada ya ugomvi uliosababishwa na mkemwenza.

Mwali Mwinyi alisema “mke mmoja wa Mfalme Haroun alitaka ujengwe msikiti na ulipomaliza fundi aliagiza akatwe mkono ndio sababu ya mgogoro watu wa fundi walikuja kulipa kisasi na ndio watu wakatawanyika na kukaa *Tumbe.* Kutokana na shuhguli zao, hutoka na kutawanyika ikifika jioni huwaoni mtu mmoja akauliza hawa wamekwenda wapi, akaambiwa hii ni” Tumbi” *Tumbe* inatokana na jina la asili “Tumbi” lenye maana ya Pakacha.

### 4.2.29 Etimolojia ya Jina la Kijiji cha Sizini

Sizini ni kijiji kilichoko katika wilaya ta Micheweni. Sizini imepakana na Tumbe Mashariki kwa upande wa Kaskazini, Kusini imepakana na Wingwi mapofu. Upande wa Mashariki ipo Bahari ya Hindi ambayo imeitenganisha na Shumba ya mjini na upande wa Magharibi imepakana na Shumba ya vyamboni na mihogoni. Kihistoria neno SIZINI lilitokana na utani wa marafiki wawili, ambapo mmoja alimtania mwenzake kwa kumwambia “Rafiki yangu wewe umekaa hapa kazi yako kuzini tu”. Katika harakati za kujitetea rafiki huyo aliikataa shutuma hiyo kwa kusema, hapana mimi SIZINI. Kwa mujibu wa mtafitiwa mwingine, Salim Khamisi alieleza kuwa ni kutokana na tabia ya wanaume ambao walimlazimisha mwanamke kufanya tendo la zinaa na akawakatalia kwa kusema mie sizini kitaalani kwa maana ya kuwa siwezi kufanya zinaa nitalaaniwa. Na ndio maana likapatikana jina hilo la Sizini hadi leo.

### 4.2.30 Etimolojia ya Jina la Kijiji cha Msuka

Msuka ni kijiji kilichopakana Konde upande wa Kaskazini na upande wa Kusini kimepakana na kinowe. Asili ya kijiji hiki kwa maelezo ya mtafitiwa bwana Hamadi Juma alisema Katika maeneo hyo palikuwa na watu wenye tabia ya uchawi na huwachukua watu uchawini kila siku. Shughuli hiyo huwa inafanywa bila watu

kujua, muhusika huwa anatoa mwanawe au mtu anaemuhusu. Siku moja mtu mmoja alikuwa tayari keshakua tayari kupeleka mtu wake wakatumwa watu wakamchukue walipofika wakaambiwa subirini kwanza namsuka. Hii ndiyo asili ya mahali hapo, yaani anasukwa nywele za kwendea safari.

#### 4.2.31 Etimolojia ya Jina la Kijiji cha Konde

*Konde* ioko wilaya ya Micheweni mkoa wa Kaskazini Pemba. Kijiji hiki kiko Mashariki ya Wete Kusini mwa Tumbe kimetengana na Gando kwa bahari ya hindi. Kwa mujibu wa maelezo ya watafitiwa asili hasa ya jina la *Konde* lilitokana na utamaduni wa kupigana. Wanajamii walioishi sehemu hii walikua na tabia ya kulewa sana gongo, tabia hii ilifuatia na mila nyengine ya kuwa wakishalewa wakipigana kwa makonde wakishindana kupigana kila walipolewa. Kutokana na mazoea hayo pali hapo pakapewa jina la *Konde* lennye maana ya ngumi.

#### 4.2.32 Etimolojia ya Jina la Kijiji cha Kinowe

*Kinowe* ni kijiji kilichoko Magharibi ya konde kijiji cha *Kinowe* kina asili ya watu ambao walikua ni washindani ya utani. Watu hawa walikua wakipigana lakini kwa visu. Pahala hapo huchukua visu vyao na ilikua hawendi pahala hapo kama huna kisu. Na unapokwenda ukiambiwa kinowe kwanza.Kutokana na kawaida ya kuambizana hivyo ndio ikawa asili ya kuitwa *Kinowe.*

#### 4.2.33 Etimolojia ya Jina la Kijiji cha Mgogoni

*Mgogoni* ni kijiji kilichoko wilaya ya Micheweni  mkoa wa Kaskazini Pemba. Kijiji hiki kiko upande wa Kaskazini ya Mashariki ya mji wa wete. Sehemu hii ni maarufu kwa kilimo cha mikarafuu. Kutokana na maelezo ya watafitiwa walisema mahali

hapa palikuwa na watu wakiishi kama sehemu nyengine za mitaa. Katika shughuli za kijamii, kulikuja kilimo cha mikarafuu wakaja watu kutoka Tanganyika na walipokuwa kazini wakipanda hiyo mikarafuu, wanawake walikua wamebeba watoto wao migongoni ndio maana pakaitwa *Mgogoni*.

### 4.2.34 Etimolojia ya Jina la Kijiji cha Mtambwe Mkuu

Mji huu ulikuwako tokea kabla ya kuja kwa wareno karne ya kumi na tisa. Kwa mujibu wa maelezo ya wasailiwa walisema asili ya hapo ni watu kutoka sehemu tofauti kama vile kutoka ushirazini. Mji huu ulisemekana ulikuwa ndani ya ngome Fulani ambayo haaikuwahi kujulikana aliyeijenga. Ulizunguushwa ukuta na ndani ndimo mlimokua na kijiji na shughuli zao kamili za kimaisha. Watu hawa walikua ni matajiri sana kuliitwa hivi kutokana na ukuu wake kila mmoja akienda hapo kumalizia shida zake. Mzee Sharifu mmoja kati ya wasailiwa alieleza walikuja wamaviti kwa maana wazungu wa kireno wakiitwa wamaviti ndio walikuja kusambaratisha ukuu wa mtambwe kwani walileta vita vya kidimu tofya tondoro banja. Wareno hawa walipoingia karne ya kumi na nane na kumi na tisa hawakujua pakuingilia walifika wakakuta mzee ambae alitoka nje ya kuta wakamwambia twataka ngoma. Kwa vile katika mji huu kulikuwa na ngoma maalumu ikichezwa Wareno walitumia mbinu hii ya kuomba kuona ngoma. Mzee Yule hakujua nia zao lakini aliwambia subirini tupange ndio ikapangwa siku wakapigiwa msewe kwani ndio ngoma ya asili ya hapo. Ngoma ilipopigwa kabuli akaimba kidimu tofya tondoo banja wao wakianza kuvunja kuta na kupiga watu. Watu wengine waliojihami walikimbilia sehemu za wete, kiuyu na kwengineko. Mpaka leo ni eneo la kihistoria ambapo wazungu huja na kutafuta taarifa tofauti. Wanajamii wa mji huu

wanajishughulisha na kazi za kilimo na biashara. Kwa hiyo asili ya jina la *Mtambwemkuu* ni kutokana na ukuu wa mji wenyewe kiutajiri na kiutawala.

### 4.2.35 Etimolojia ya Jina la Kijiji cha Mzambarauni Takao

Jina la mahali hapa limetokana miti hii ya mizambarau. Kutokana na maelezo ya baadhi ya watafitiwa, walisema Jina la Mzambarauni takao limetokana kwamba palikuwa na bibi mmoja anafanya dawa za kienyeji za watoto na wanawake. Bibi huyu alijipatia umaarufu kwa uzuri wa dawa zake, kwani zilitibu vizuri sana lakini kukawa kuna baadhi ya wateja hawakufanikiwa. Watu hao wakaamua kwenda kumwambia mbona sisi hatujafanikiwa bibi akawaambia mimi dawa zangu nawapa niwatakao. Kwa maana hiyo wanajamii wakawa wanapoulizwa mwendea wapi hujibu twenda Mzambaruni kule kwa watakao. Kwa mujibu wa maelezo haya jina la Mzambarauni Takao limetokana na miti ya mizambarau pamoja na maneno ya bibi ambaye alikuwa ni mtabibu wa dawa za asili.

## 4.3 Vigezo vya Utoaji Majina ya Mahali ya Kaskazini Pemba

Majina ya mahali hutolewa kulingana na vigezo mbalimbali kama majina ya miti, majina ya watu maarufu, hali ya nchi, matukio yakihistoria shughuli zakijamii, hali za kimaisha/uchumi na hata itikadi za kijamii. Ufafanuzi wa Vipengele hivi umeainishwa hapo chini kama ifuatavyo:-

### 4.3.1 Majina ya Mahali Yanayotokana na Mimea/Miti

*Mitiulaya*: Linatokana na miti maalumu iliyoaminiwa kuwa asili yake ni kutoka Ulaya kama mtafiti alivyodokeza kwenye (4.2.5)

*Muharitani*: Linatokana na jina la mti unaoitwa muharita, kama ilivyodokezwa na mtafiti kwenye (4.2;11)

*Muembebutu*: Linatokana na mti ulioitwa muembe, uliokuwa umetolewa matawi na kuwa butu.

*Mbuyugowe*: Gowe ni msamiati wa Kipemba cha zamani uliokuwa na maana ya vita, mzozo au ugomvi. Kulikuwa na mbuyu kwenye sehemu maalumu ambayo watu wa kijiji hicho wakikutana kama sehemu ya mahakama ya jadi kujadili mizozo iliyopo baina ya wana jamii. Sehemu hiyo kwa hivyo ikaitwa Mbuyugowe, kwa maana ya mbuyu wa mizozo. Kwa hivyo jina Mbuyugowe linatokana na mti ulioitwa mbuyu.

*Mzambarauni Takao:* Ni jina lililotokana na mti ulioitwa mzambarau. Miti ya aina hii ipo kwa wingi kisiwani Pemba. Hadi leo sehemu ya Mzambarauni miti hii inapatikana kwa kiwango kikubwa sana.

*Kibuyuni*: Kibuyu ni udogoshi wa mbuyu. Jina hili liko chini ya ngeli (ki-v). Kihistoria inasemekana sehemu hii ilkuwa na kibuyu kidogo, ndiyo ikaitwa kibuyuni.

*Michungani*: Sehemu hii ilikuwa na miti ya miba iliyoitwa michunga na eneo likaitwa Michungani.

*Mianzini*: Sehemu hii ilikuwa na miti iliyoitwa mianzi na kwa hivyo eneo likaitwa Mianzini.

### 4.3.3 Majina ya Mahali Yaliyotokana na Watu Maarufu

*Kwa setimende* Jina hili lilitokana na tajiri mmoja wa Kihindi aliyeitwa Setimende.

*Kwa Machozi*: Jina hili lilitokana na tajiri mmoja wa Kiarabu, aliyeitwa kwa jina la uchokozi kutokana na ugonjwa wa macho aliokuwa nao. Mwarabu huyu alikuwa akitokwa na machozi kwa wingi na kwa hivyo dukani pake pakaitwa kwa Machozi.

*Kwa Nondo*: Nondo ni jina la utani la tajiri wa Kipemba aliyeishi huko Kiuyu Mbuyuni, wilaya ya Micheweni Pemba. Eneo hili lilipewa jina kwa Nondo ili kuakisi jina la tajiri huyu.

*Kwa Shaame Mata*: jina hili linatokana kiongozi wa jadi wa wakati huo aliyeitwa Shaame Mata.

### 4.3.4 Majina ya Mahali Yanayotokana na Mazingira/ Hali ya Nchi

Kutokana na data zilizokusannywa, yapo majina ya mahali yaliyotokana na muenekano wa hali ya nchi ama mazingira ambayo yanatokana na maumbile ya kijografia. Mjina hayo ni kama yafuatayo; yalivyonukuliwa na mtafiti wakati wa mahojiano na watafitiwa wake.

*Kilimajuu*: Jina hili linatokana na kilima kilichonyanyuka juu kidogo. Kilima hiki kiko nje kidogo ya mji wa Wete; njiani kuelekea Gando. Eneo hili Wapemba huliita Kilimajuu.

*Kilimandege:* Ni juu ya kilima kuelekea Wete Bandarini. Eneo hili lilikuwa na miti ya mauwa. Ndege wengi walikuja kujipatia burdani ya upepo wa miti na asali ya maua ambayo ni chakula kimoja wapo cha baadhi ya ndege hao. Kwa sababu hii eneo hili lkajipatia jina la Kilimandege.

*Kilimahewa:* Jina hili linatokana na muinuko kidogo uliopo katika kijiji na hali ya hewa ilikuwa ni ya upepo.

*Kidutani:* Ni eneo lililoinuka kama mlima kutokana na kuwa juu kuliko maeneo mengine ndio likatolewa jina la kidutani.

*Gongoni:* Gongo ni muinuko uliopinda kidogo ukatoa mfano wa mgongo na jina likatolewa kutokana na aina ya muinuko huo.

*Mchangani*: Hii ni sehemu iliyo na mchanga mwingi.

### 4.3.5 Majina ya Mahali Yanayotokana na Itikadi

*Micheweni:* Ni jina lilitokana imani za kishirikina.

*Kidundo uchawi:* Nijina lililotokana na imani za kishirikina

*Kipangani:* Ni jina lililotokana na imani ya kishirikina ambapo panga ni sehemu ambayo watu huabudu na kueka vyano kwa ajili ya mashetani.

### 4.3.6 Majina Yanyotokana na Vyakula/Vinywaji

*Majimbikani*: Ni jina linalotokana na aina ya chakula cha nafaka.

*Maziwang'ombe:* Jina linatokana na kinywaji.

*Njuguni:* Ni jina lililotolew kwa sababu ya kuwepo kwa njugu yaani karanga katika eneo hilo.

### 4.3.7 Majina ya Mahali Yanayotokana Hali za Kiuchumi za Jamii

*Maskini hajengi:* Ni jina linaloonesha hali za kijamii katika kipato kwani mtaa huu huwa unanyumba za kitajiri maskini hawezi kupata eneo akajenga.

*Chasasa:* Mtaa huu unaonesha jinsi ya hali ya miji kubadilika kutoka hali duni kwenda hali ya juu.

*Majenzi*: Ni nyumba za kisasa zenye mitindo ya kifahari.

### 4.4 Majina ya Mahali Yanayoakisi Utamaduni wa Wapemba

Utamaduni ni maisha ya mtu au jamii katika mazingira maalumu ya asili yanayojumuisha lugha mama, imani, mila, maadili, itikadi, desturi, sanaa, michezo na mazingira au mahali mahsusi (BAKIZA, 2008). Hivyo basi kutokana na tafsiri hii majina ni miongoni mwa maneno yanayojenga lugha ambayo ni kipengele cha utamaduni. Kwa muktadha huu inaonekana kuwa majina ya mahali na hata watu yanaakisi utamaduni wa wanajamii husika. Kuna baadhi ya majina ya mahali yanaakisi moja kwa moja utamaduni wa Wapemba. Baadhi ya majina hayo yameainishwa na mtafiti hapo chini.

### 4.5 Maziwang'ombe

Maziwang'ombe ni jina linalotokana na asili ya kuwepo kwa maziwa mengi yanayozalishwa katika kijiji hiki. Wanajamii wa mahali hapa walikuwa na utamaduni wa ufugaji wa ng'ombe wengi kiasi ya kuzalisha maziwa mengi. Kila mwanakijiji huwa na ng'ombe wasioupungua sita hivyo jina linautambulisha utamaduni wa asili wa Wapemba wa eneo hili. Kwa hivyo jina Maziwang'ombe linatokana na utamaduni na kazi iliyokuwa ikifanywa na watu wa eneo hilo; kazi ya kufuga ng'ombe waliokuwa wakizalisha maziwa kwa wingi sana.

#### 4.5.1 Micheweni

Jina Micheweni linautambulisha utamaduni wa asili wa eneo hili. Limejengeka zaidi kwa misingi ya imani na itikadi. Wanajamii waliamini kwamba mahalia hapa palikuwa na watu makatili sana. Watu hawa walikuwa na desturi za uchawi. Wanajamii wa vijiji vyengine waliwaogopa sana kutokana na tabia yao ya ushirikaina na uchawi. Mahali hapo paliitwa Michawini yaani mahali pa uchawi na

baadae jina likageuka likawa Micheweni. Kwa ufupi tunaweza kusema kwamba jina la *Micheweni* linatokana na desturi na tabia mbaya ya ushirikina na uchawi anbayo ilikuwa ni sehemu ya utamaduni wa watu hawa. Maelezo haya yanaakisi nadharia ya ujinaishi inayotambulisha majina ya watu kutegemeana na utamaduni wao. Kwa hapa jina limekuja kutokana na utamaduni wa watu waliokuwa wakiishi eneo hili, tabia ya uchawi na ushirikiana, kwa sababu hii eneo hili liliitwa *Micheweni* .

### 4.5.2 Gombeume

Mahali hapa palikuwa na kiwanja maalumu kwa ajili ya mchazo wa ng'ombe. Mchezo mashuhuri sana Kisiwani Pemba kwa wakati huo. Ulikuwa ukichezwa kwa kutumia ng'ombe wa jinsi zote; majike na madume. Ngombe aliyesifikana sana kwa uhodari na kuvuta hisia za watu wengi ni ng'ombe dume maalumu aliyeitwa *Gombeume*. Jina la ng'ombe huyu likatumika kupaita mahali palipokuwa pakichezewa mchezo huo wa ng'ombe. Jina hili liliakisi moja kwa moja utamaduni wa Wapemba wa kucheza mchezo wa ng'ombe.

### 4.5.3 Mchangamdogo

Wanajamii wa eneo hili walifanya kazi kwa pamoja na kuchangiana fedha na rasilimali nyengine, ili kila mmoja aweze kukamilisha majukumu yake ya kimaisha. Mwanajamii alitakiwa kutowa mchango ingawa mdogo ili kufanikisha jambo la mwenzake. Mchango uliotolewa na mwana jamii uliitwa mchango mdogo. Eneo hili kwa sababu hii likaitwa mchango mdogo, likageukageuka na sasa limekuwa *Mchangamdogo.* Kwa ujumla tunaweza kusema kwamba, jina hili limetokana na utamaduni wa Wapemba wa kuchangiana kidogo kidogo kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli zao.

### 4.5.4 Majimbikani

Majimbi ni aina ya viazi vinavyolimwa kiasiwani Pemba. Eneo linaloitwa Majimbikani lilikuwa mashuhuri sana kwa kilimo cha aina hiyo. Watu walipaita *Majimbikani*, wakiwa na maana ya kuwa, hii ni sehemu yenye kulimwa majimbi kwa wingi. Kwa ujumla tunaweza kusema kwamba, jina hili linatoka na utamaduni wa Wapemba wa kilimo cha majimbi, kilichoshamiri enzi hizo.

### 4.5.5 Ngagu

Ni jina la kijiji ambacho kiko katika kisiwa kidogo cha Fundo kilichopo Kaskazini Pemba. *Ngagu* ni msamiati wa kidigo unaotumika kumuita samaki ambaye Upembani huitwa kuwi. *Ngagu* kwa sasa ni jina la kijiji kilicho kwenye diko ambalo wavuvi wa Fundo kwa wakati huo wakifikia wakiwa na idadi kubwa ya Samaki waitwao *Ngagu* au kuwi. Kwa ufupi, tunaweza kusema kwamba jina hili lilikuja kutokana na utamaduni wa Wapemba wa kuvua samaki.

### 4.5.6 Msuka

Watafitiwa wa kazi hii waliohojiwa na mtafiti mnamo Aprili (2015) walisema kwamba, wanawake wa Kipemba wana tabia na dasturi ya kusuka nywele zao kwa mitindo tofauti. Misuko ya nywele huitwa kwa majina tofauti tofauti. Ipo misuko iitwayo minyoosho, tandika, kawa, kijicho cha mke mwenza, chana la ndizi na mingi mingineyo. Wakati mwingine ndani ya misuko hiyo huwekwa maua au behedani na mara nyengine kala zilizokuwa na muundo wa vitana. Misuko hii husukwa siku za sikukuu na sherehe nyengine na mara nyengine Wapemba husuka misuko hiyo wakiwa wanajitayarisha kwa safari za hapa na pale. Eneo ambalo Wapemba

walifuata utamaduni huu kwa kiwango kikubwa zaidi liliitwa Msuka kuakisi utamaduni wa kujiremba na kusuka nywele.

### 4.6 Mjadala wa Matokeo ya Utafiti

Matokeo ya utafiti huu yametuwezesha kufikia lengo la kuitafiti mada hii lililohusu kuchunguza etimolojia ya majina ya mahali ya Kaskazini Pemba kuwa kitambulisho cha utamaduni wa Wapemba. Lengo hili lilifanikiwa kutokana na taarifa tulizozikusanya kupitia malengo mahususi ya utafiti huu ambayo ni kubainisha etimolojia ya majina ya mahali yanayopatikana Kaskazini Pemba, kufafanua vigezo vinavyotumika kutoa majina ya mahali ya Kaskazini Pemba na kubainisha utamaduni wa Wapemba jinsi ulivyoakisiwa na majina ya mahali ya Kaskazini Pemba.

Tulichogundua kutokana na taarifa za utafiti huu ni kuwa utambulisho wa utamaduni wa jamii yoyote umekitwa kwenye mfumo wa maisha ya jamii hiyo. Tunaweza kuitambua jamii fulani iwapo tutaangalia kwa kina namna wajishughulishavyo na wahusikavyo katika nyanja zote za maisha yao. Vipengele anuai vinavyofungamana na jamii yoyote ni kielelezo thabiti cha kuipambanua na kuitambulisha jamii husika. Majina yanazo taarifa nyingi zihusianazo na jamii inayotumia majina hayo. Al Zumor (2009:16) anafafanua kuwa "*leksimu zilizomo katika majina ya watu ni ushahidi toshelevu juu ya tabia na mawazo ya jamii husika, zikionesha wazi wazi asili ya watu na ujuzi wao, itikadi, mitindo na hadhi yao kijamii, n.k.*" Majina yanaakisi na kusisitiza utambulisho yanapotolewa na hata yanapopokea mabadiliko (Zawawi, 1998).

Majina ya mahali hayatolewi kiholela. Huzingatia na kuakisi masuala mbalimbali ya kijamii. Matukio ya kihistoria, shughuli za kijamii, watu maarufu, hali ya hewa na mazingira, na mengineyo ni vishawishi vinavyochochea uibukaji wa majina ya maeneo. Matokeo ya utafiti huu yamethibitisha kuwa kupitia majina ya maeneo ya Kaskazini Pemba unaweza kufahamu kwa kina masuala kadhaa ya kiutamaduni yanayofungamana na jamii ya Wapemba wa Kaskazini. Hivyo basi, suala la utoaji majina linahitaji kuthaminiwa na kuenziwa ili kutunza amali hii muhimu ya jamii ya Wapemba.

## 4.7 Hitimisho

Sura hii imeangalia uchanganuzi wa data na mjadala wa matokeo ya utafiti. Mtafiti amechanganua data kulingana na malengo na maswali ya utafiti. Data za watafiwa zilichanganuliwa kufuata mbinu ya maelezo na kujadiliwa kwa maelezo.

# SURA YA TANO

# MUHUTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Sura hii inawasilisha muhtasari matokeo na hitimisho la utafiti huu. Aidha mtafiti alichunguza majina ya mahali na kuona yanavyoutambulisha utamaduni. Pia alitoa mapendekezo kutokana na namna alivyoona matokeo ya utafiti huu.

## 5.2 Muhutasari wa Matokeo ya Utafiti

Utafiti huu umechunguza majina ya mahali kuwa utambulisho wa utamaduni wa Wapemba Kaskazini. Katika kufanya utafiti huu malengo matatu yaliongoza utafiti huu. Malengo hayo yaliweza kupimwa kupitia zana na mbinu mbali mbali zilizotumika.

Malengo hayo ni kama yafuatayo:

1. Kubainisha etimolojia ya majina ya mahali yanayopatikana Kaskazini Pemba.
2. Kufafanua vigezo vinavyotumika kutoa majina ya mahali ya Kaskazini Pemba.
3. Kubainisha utamaduni wa Wapemba jinsi ulivyoakisiwa na majina ya mahali ya Kaskazini Pemba.

Kutokana malengo hayo mtafiti aliongozwa na maswali. Katika kujibu maswali hayo, aligundua kuwa majina ya mahali yana asili na sababu za kuitwa kwa majina hayo mahali hapo na pia huwa yanatokana na jamii husika shughuli zao, imani na hata tabia ya mtu. Hivyo maswali ya utfiti  yalienda sambamba na malengo, mtafiti alibainisha majina ya mahali yaliyopatikana Kaskazini Pemba na kuyatolea asili zake. Pia majina hayo yalibainika kuwa yanatokana na utamaduni wa jamii iliyopo

na ndio inayowatofautisha kati ya mahali pamoja na pengine. Misingi ya utafiti huu ni kuhusu etimolojia ya majina ya mahali kuwa u Matokeo ya utafiti huu yameonesha kuwa majina ya mahali yanaakisi utamaduni wa Wapemba. Kwa mantiki hiyo mtafiti anapendekeza kufanyika kwa tafiti nyengine katika majina ya maeneo mengine kama mashamba, mito, miti, na vyakula kuangalia yanavyochangia msamiati wa lugha ya Kiswahili na lahaja za maeneo hayo. Pia kufanya utafiti ambao utachunguza sababu zinazochangia kuibuka kwa majina mapya ya mahali katika jamii. Lengo la utafiti huo liwe ni kuchunguza sababu za kuibuka kwa majina ya mahali katika jamii na athari zinazopatikana kwa wanajamii kuacha kutumia majina ya asili ya mahali hapo.

Mwisho mtafiti ana pendekeza idara ya Mambo ya kale iwe na jalada maalum linalohifadhi majina ya mahali na asili zake. Kwani majina ya mahali yana umuhimu wake kwa vile yanarahisisha kupata kile ulichohitaji kwa wakati ule, pia yanatambulisha utamaduni wa jamii husika kwani unapotajiwa hawa ni watu wa mahali fulani unajua kama wana tabia gani na maisha yao ni vipi. Utamaduni huo ilikua ni shughuli zinazofanywa na jamii kama vile kilimo, ufugaji mila desturi ambazo wanajamii wengi wanazo.

## 5.3 Hitimisho la Utafiti

Utafiti huu ulichunguza etimolojia ya majina ya mahali Kaskazini Pemba kuwa utambulisho wa utamaduni. Mtafiti alichunguza etimolojia ya majina ya mahali yaliyopatikana kaskazini Pemba kwa kuongozwa na lengo na maswali ya utafiti huu. Matokeo ya utafiti huu yameonesha kuwa majina ya mahali ya Kaskazini Pemba yanautambulisha utamaduni wa Wapemba. Hivyo imependekezwa kuwa majina ya

mahali yaangaliwe kwa jicho la upekuzi kwani yana umuhimu mkubwa katika kueleza historia mbali na kuwa ni utambulisho wa jamii. Kufanyike tafiti zitazozingatia athari za kuibuka kwa majina mapya na kuachwa yale ya asili.

## 5.4 Utoshelevu wa Nadharia Iliyotumika

Kutoana na nadharia ya *jumuishi* ya Gille's, mtafiti aliweza kugundua kuwa majina ya mahali yanatokana na matukio ya jamii pamoja na shughuli zinazofanywa na wanajamii. Hivyo mtafiti kwa kutumia nadharia hii, aliweza kuelezewa matendo mbali mbali ya wanajamii yanayoitambulisha jamii ambayo yalimsaidia mtafiti uchambuzi na uwasilishaji wa data. Vile vile nadharia ilisaidia katika kujibu maswali yaliyoongoza utafiti huu, Kwani imeonesha jinsi majina yalivyoweza kuutambulisha utamaduni wa jamii. Pia imeonesha matumizi ya majina hayo katika kuwepesisha mawasiliano katika jamii. Hivyo nadharia ya utambulishi ilikuwa muhimili na dira ya kumulika matendo ya kijamii yanavyoakisi utoaji wa majina ya sehemu wanazoishi.

## 5.5 Mapendekezo Juu ya Tafiti Zijazo

Maelezo kuhusu majina na utambulisho yameelezwa na watu mbali mbali. Mtafiti amezungumzia kuhusu majina ya mahali yanavyokuwa kitambulisho cha utamaduni wa Wapemba Kaskazini. Mtafiti mebaini kuwa kipengele cha majina ya mahali nacho kinahitaji kuangaliwa kwani imegundulika kuwa majina ya mahali ni moja wapo ya vipengele vinavyoutambulisha utamaduni wa jamii. Hivyo imependekezwa kwa tafiti zijazo kujihusisha na athari za majina ya mahali yanayobadilika. Na pia maumbo ya majina ya mahali katika kipengele cha mofolojia na fonolojia kinaweza

kufanyiwa utafiti kuona jinsi wanajamii wanatumia lugha kwa kila kipengele cha maisha.

## 5.6 Hitimisho

Kwa muhutasari sura hii ilitoa majumuisho kuhusu utafiti huu, muhutasari wa matokeo ya utafiti huu pamoja na mapendekezo ya tafiti zijazo.

**MAREJELEO**

Adam, J. na Kamuzora, F., (2008), *Research Methods for Buisiness and Social Studies* Morogoro: Mzumbe Book Project

Ally, J. na Mustafa, (1930), *Nahau-Al-Waadhih. Daaru Maarifa: Misri.*

Al-Zumor, A. Q. G., (2009), *A Social-Cultural and Linguistic Analysis of Yemeni Arabic Personal Names,* Abha: King Khaled University.

Backhaus, P., (2007), *Linguistic Landascapes: A Comparative Study, Urban multilingualism in Tokyo,* Great Britain: MPG Book ltd

Baitan, B., (2010), *Morphosemantic Analysis of Ruhaya Person Names* (Unpublished M.A Dessertation), Dar es Salaam: University of Dar es Salaam.

BAKIZA (2008), *Utamaduni wa Mzanzibar,* Zanzibar: BAKIZA.

Baver, H. D. R., (1979), *Chinese Family and Kinship,* Newyork: Colombia University Press

Best, J. W. na Kahn, J. V., (1993), *Research in Education.* United State of America: Allyn and Bacon.

Boas, F., (1964), *"On Geographical Names of the Kwakiuti Indians"Language in Culture and Society, A Reader in Linguistics and Anthropology*. New York, Evaston and London, University of calfonia, Berkeley Harper and Row Publishers.

Buberwa, A. (2010*), Investigating of Sociolinguistic Aspects of Place Names in Ruhaya in North-West Tanzania, Unpublished M. A Dissertation*. University of Dar es Salaam

Cameroon, K (1961) *English Place Names*.London, Exford University Press.

Chum, H. (1982*), Desturi na Mila Zetu*.East Africa  Publication Limited Arusha.

Chulk, O. O (1992), *Names fromAfrica: Their Origin, Meaning and Pronoucition,* Chicago, John Publishing co Cooper

Edelman, L., (2010), *Linguistic Landscapes in the Nertherlands: A Study of Multilingualism in Amsterdam and Friesland,* Amsterdam: LOT.

Enon, D. C., (1998), *Educational Research, Statistics and Measurements,* Uganda: Department of distance Education, Makerere University

Khamis, A. M na Madumula, J. S., (1989), *"Majina Yanayohusu Watu"* Mulika o.21, Dar es Salaam TUKI Kofi, A (2006), "The Sociolinguistic of Akan Personal name", In Nordric Journal of African Studies, 15(2): pp.206-235

Kombo, D. K and D. L Tromp (2006), *Proposal and thesis Writing: An Introduction*. Nairobi, Paulines Publications Afrika

Kofi, A (2006)*, "The Sociolinguistic of Akan Personal name",* In Nordric Journal of African Studies, 15(2):pp.206-235

Kothari, C.R (2009), *Research Methodology.Method and Techniques,* Second Revised Edition, New Age International (P) ltd: New Delhi.

Massamba D. P. B., (2004) *Sarufi Maumbo Ya Kiswahili Sanifu*.Taasisi Ya Uchunguzi wa Kiswahili Dar es Salaam

Manyasa, J. (2008*), Investigating the Basis of Naming People in Kisukuma, Unpu*blished M.A. Dessertation, University of dare s salaam

Mlacha, S. A. na Hurskainen (1995), *Lugha, Utamaduni na Fasihi Simulizi ya Kiswahili*: Dar es Salaam.

Msanjila, Y. P. na Wenzake (2009), *Isimu Jamii, Sekondari na Vyuo*. Tasisi ya Uchunguizi ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Musere, J. (2000*) Traditional African Names*. Lanham, Marrylanda and Landy The Scarecrow Press, Inc.

Mutembei, A. K. (2009), *UKIMWI Katika Fasihi ya Kiswahili* .Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Chou Kikuu Dar es Salaam.

Muzale, H. R. T., (1996*) Linguistic and Social-Culture Aspects in Interlacanstrine Bantu Names*" Kiswahili Vol.61.28-49

Omary, C., and I. A. Richerds (1966), *"Person Names in Social-Cultural Context"* Jarida la Kiswahili la Chuo cha Uchunguzi wa Lugha ya Kiswahili (Journal of the Institute of Swahili Research), Vol.40/2 sep,1970,Dar es Salaam Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam

Opie, C.(2010*),Doing Education Research, Roliver's* Yard 55 City Road London

Redio Nour (18/10/2013*), Kipindi cha Tutunze Historia Yetu Redio Zanzibar*: Nour.

Saluhaya, M. C., (2010), *Kiswahili-1, Nadharia ya Lugha Kidato cha Tano na Sita*.Children Education Society: (CHESO) Dar es Salaam.

Schotsman, P., (2003*) A Grammar of Runyambo Language of Tanzania* (LOT) Project Universityu of Dar es Salaam. LOT Publisher Grammar Series No.1

Seif, D. G., (2011) *Nyimbo za Jando katika Jamii ya Kikaguru, Kata ya Gairo,* Tasnifu M.A. Kiswahili.

Sengo, T. S. Y., (2009*), Sengo na Fasihi za Kinch*i. Al-amin Education and Research Academy: Dar es Salaam.

Zawawi, Sh. M., (1998), *African Muslim Names: Images And Identities*, England: Africa World Press.

Zawawi, Sh. M., (1993), *What's in a Name? Unaitwaje? A Swahili Book of Names*, England: Africa World Press.

**KIAMBATISHO** Na 1

Maswali ya Usaili kwa watafitiwa

(Maelezo binafsi)

1..................................................Jinsia.......................................

Umri ..................................................................Elimu.......................................

Kazi.....................................................................Tarehe/.......................................

2. Unaishi mtaa gani?..........................................................................................

Taja mitaa mingine mine unayoifahamu

i).......................................ii).......................................iii).......................................

iv)..................................................

3. Kawaida kila jina la mahali lina asili toa maelezo mafupi kuhusu mitaa mitatu unayoijua.asili zake.

i)Mtaa.....................................................................................

a)Umeanza lini.?..................................................................................................

b)Chanzo chake ni nini?...............................................................................................

i)...................................................................................................................................

.....................................................................................................................................

.....................................................................................................................................

..

ii).................................................................................................................................

.....................................................................................................................................

.....................................................................................................................................

...................................................................................................................

4.Majina haya yana umuhimu kwa wana jamii ?Yana faida au hukumbusha tukio la kihistoria? Kitambuu ..........................................................................................

..........................................................................................................................

Dodeani...................................................................................................................

..........................................................................................................................

.

Pandani...................................................................................................................

..........................................................................................................................

6 Majina ya mahali yana miundo tofauti ya lugha. Kuna iliyo na majina ya miti,wanyama, muambatano wa majina,sitiari,

a) Orodhesha majina matatu yenye majina ya miti/mimea na ueleze kwa nini ukaitwa jina hilo.

i).......................................................................

ii)......................................................................

iii).........................................................................

b) Taja mitaa minne yenye majina ya wanyama.na toa maelezo kwa nini ikaitwa majina hayo

i)............................................................................................

ii)............................................................................................

c) Taja mitaa miwili iliyo na majina ya vitu toa sabu za kuitwa majina ya vitu.

7. Kuna umuhimu gani wa kupewa majina hayo?

8. Majina hayo yanatambulisha nini katika jamii ya Wapemba?

AHSANTE SANA

## KIAMBATISHO Na. 2

### MWONGOZO WA MASWALI YA HOJAJI KWA WAZEE WA VIJIJI VYA KASKAZINI PEMBA VILIVYOTEULIWA KATIKA UTAFITI HUU

**MADA**: ***Etimolojia ya Majina ya Mahali ya Kaskazini Pemba Kuwa Kitambulisho cha Utamaduni wa Wapemba***

Mtafiti ………………………………………………………… Tarehe …..........………

- Tunaomba utueleze kwa kifupi kuhusu jina lako, umri wako, kijiji unachoishi, kiwango chako cha elimu na shughuli ufanyayo?
- Tunafanya utafiti kuhusu ***Etimolojia ya Majina ya Mahali ya Kaskazini Pemba Kuwa Kitambulisho cha Utamaduni wa Wapemba***. Tunaomba ushirikiane nasi kwa kutupatia taarifa zifuatazo;

---

1. (a) Majina ya sehemu wanazoishi watu hutolewa kwa sababu na chanzo maalumu. Una maoni gani kuhusu hoja hii?

   (b) Kila jina huwa na maana na asili yake. Unasemaje kuhusu hoja hii?

2. Tutajie majina ya vijiji vitano tu vilivyoko karibu na kijiji chako unavyoamini kuwa tunaweza kupata taarifa kuhusu maana, sababu na asili au chanzo cha jina hilo?

3. (a) Yako majina ya vijiji yanayotokana na watu maarufu, matukio ya kihistoria, hali ya kimazingira au kijiografia na shughuli zifanywazo na watu. Tutajie majina ya vijiji vya karibu na kijiji chako yenye mwelekeo huo.

(b) Taja vigezo vya utoaji wa kila jina la kijiji utakalolitaja na fafanua taarifa za kihistoria au mnasaba wa jina hilo.

4. Tutajie majina ya vijiji yenye taarifa kuhusu utamaduni wa Wapemba na fafanua taarifa hizo za kiutamaduni.

5. Toa maoni yako ya jumla kuhusu etimolojia ya majina ya mahali ya Kaskazini Pemba kuwa kitambulisho cha utamaduni wa Wapemba

*****************Tunakushukuru sana kwa mchango wako*****************

## KIAMBATISHO NAMBA 3

MAJINA YA MAHALI YALIYOCHUNGUZWA ASILI ZAKE

Gando

Wete

Jadida

Sebuwatu

Majimbikani

Mitiulaya

Kilimandege

Kipangani

Kilimahewa

Nyongehajengi

Bopwe

Tangilamaji

Muharitani

Utaani

Chasasa

Junguni

Misooni

Chaoni

Kenya

Kidutani

Ngadu

Ndooni

Uondwe

Kiapaka

Mpaka njia

Mtambwemkuu

Kidundouchawi

Uzunguni

Muembebutu

Njuguni

Mianzini

Mapofu

Kinazini

Shumbavyamboni

Kijuki

Mvimbe

Mchangani

Kitambuu

Kibuyutondo

Pangamsikiti

Wingwi

Mjini wingwi

Pandani

Mgogoni

Kinowe

Madebeni

Miwani

Kwashehambwarahaji

Kojifa

Jindaoge

Dodeani

Mzambarauni